**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA, 2024/2025

**MHE. SHAIB HASSAN KADUARA**

**JUNI, 2024**

# YALIYOMO


Yaliyomo ................................................................................................ i

Orodha ya Viambatisho ................................................................................ ii

Vifupisho vya Maneno ................................................................................. iii

1.0 Utangulizi ............................................................................................ 1

2.0 Utekelezaji wa Programu za Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Kipindi cha Miezi Tisa (Julai – Machi) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ................... 3

3.0 Mafanikio ya Utekelezaji wa Programu za Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Kipindi cha Julai – Machi, 2023/2024 ....................................................... 5

4.0 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya WMNM .................................... 29

5.0 Mwelekeo wa Bajeti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ........................................................................................... 37

6.0 Maombi ya fedha kwa kazi zilizopangwa kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 ........................................................................................... 43

7.0 Hitimisho ............................................................................................ 44

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Namba.1: Mapitio ya Upatikanaji wa Fedha kwa kazi za kawaida kwa Mwaka wa Fedha2023/2024 ........................................ 46

Kiambatisho Namba.2: Maeneo yaliyoimarishwa huduma ya umeme kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024 .......................................... 48

Kiambatisho Namba.3: Hali ya uingizaji na matumizi ya Mafuta kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2024........................................................ 49

Kiambatisho Namba.4: Bei za mafuta ..................................................................... 50

Kiambatisho Namba.5: Hali ya Uingizwaji na Matumizi ya Gesi kwa Kila Kampuni......................................................................... 50

Kiambatisho Namba.6: Idadi na aina ya malalamiko yaliyopokelewa na kutatuliwa....................................................................... 51

Kiambatisho Namba.7: Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025............................................................... 52

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| WMNM | Wizara ya Maji, Nishati na Madini |
| KV | Kilovoti |
| MW | Megawatt |
| TANESCO | Tanzania Electricity Supply Corporation (Shirika la Umeme Tanzania) |
| STAMICO | Shirika la Taifa la Madini |
| TZS | Tanzania Shillings |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan (Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar) |
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| ZAWA | Zanzibar Water Authoriy (Mamlaka ya Maji Zanzibar) |
| ZECO | Zanzibar Electricity Corporation (Shirika la Umeme Zanzibar) |
| ZURA | Zanzibar Utility Regulatory Authority (Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar) |

## 1.0 UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha hoja katika Baraza lako Tukufu kwa lengo la kupokea, kujadili, kuzingatia na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

2. **Mheshimiwa Spika,** naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwa kutujaalia neema ya uhai, afya njema na uwezo wa kukutana leo hii kwa lengo la kujadili Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi) 2023/2024 pamoja na kuwasilisha Mwelekeo wa Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa dhamira ya kuendelea kuwatumikia wananchi wote wa Zanzibar.

3. **Mheshimiwa Spika,** naomba kwa heshima kumpongeza Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti na makini katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wake ndani ya Serikali ya Awamu ya Sita.

4. **Mheshimiwa Spika,** pongezi za dhati ziende kwa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuimarisha uchumi, umoja na mshikamano kwa wananchi wote. Kadhalika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wasaidizi wake wakuu; Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa namna wanavyoendelea na majukumu yao ya kumshauri vyema Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

5. **Mheshimiwa Spika,** katika kufanikisha majukumu ya kitaifa kwa ujumla, wananchi tunaridhishwa na uongozi wao ambao umeiwezesha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuitekeleza vyema Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2020-2025 unaokwenda sambamba na malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020-2050 pamoja na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) wa mwaka 2021-2026.

6. **Mheshimiwa Spika,** nakushukuru wewe binafsi kwa umakini na umahiri wa kuliendesha Baraza lako Tukufu, pia nawapongeza Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza lako Tukufu pamoja na Wenyeviti wa Kamati na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu na Watendaji wa Baraza la Wawakilishi kwa kuendelea kushirikiana na sisi na kutuongoza katika kutekeleza vyema majukumu yetu.

7. **Mheshimiwa Spika,** pongezi za pekee ziwaendee Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati, Mheshimiwa Yahya Rashid Abdalla; Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Kwahani na Mheshimiwa Aza Januari Joseph; Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii kwa busara, hekima na uzoefu wao unaotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi na kuweza kutatua changamoto katika jamii zinazohusu Sekta ya Maji, Nishati na Madini. Aidha, pongezi ziende kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma pamoja na Wajumbe wake wote kwa kuendelea kutusimamia katika utekelezaji wa mipango ya Wizara katika bajeti yetu ya Mwaka wa Fedha 2023/2024.

8. **Mheshimiwa Spika,** nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Shaaban Ali Othman Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Mpendae ambaye aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini, kwa kuteuliwa kuwa Waziri katika Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Hakika busara, umahiri na juhudi zake za kuwaletea maendeleo wananchi zimempelekea Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuendelea kumuamini na kumpa dhamana ya kumsaidia katika Wizara hiyo ambayo ni muhimili wa maendeleo ya nchi yetu.

9. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, nimpongeze Mheshimiwa Zawadi Amour Nassor Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Konde kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri katika Wizara ya Maji, Nishati na Madini. Nimuahidi kuwa niko tayari kumpa ushirikiano pamoja na watendaji wangu katika kuwapatia wananchi huduma zilizo nafuu, bora na za uhakika.

10. **Mheshimiwa Spika,** kwa heshima naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuendelea kuniamini katika nafasi ya Waziri wa Maji, Nishati na Madini wa Serikali ya Mapinduzi

ya Zanzibar. Hii ni heshima kubwa kwangu binafsi kuiongoza Wizara inayogusa maisha ya kila mwananchi. Naahidi nitaendelea kuitumikia nafasi hii kwa nguvu zangu zote katika kuwaletea maendeleo wananchi na kuhakikisha huduma za maji, umeme, mafuta na maliasili zisizorejesheka zinapatikana na zinaimarika.

11. **Mheshimiwa Spika,** pia, nawapongeza wananchi wa Zanzibar kwa imani na upendo wa dhati katika kumuunga mkono Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake za kuiletea maendeleo Zanzibar. Pongezi hizi maalumu pia ziende kwa wananchi wa Jimbo la Chake Chake kwa kuendelea kuniamini na kunichagua kuwa Mwakilishi wao. Nawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia na kushirikiana nao katika kuleta maendeleo na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazolikabili Jimbo letu. Wito wangu kwa wananchi wote wa Zanzibar waendelee kumuunga mkono na kushirikiana nae kikamilifu kwa maslahi ya Taifa.

12. **Mheshimiwa Spika,** baada ya shukurani hizo, naomba uniruhusu kuwasilisha Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi, 2023/2024) na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Hotuba hii imezingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020 – 2025, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050; Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar 2021 – 2026; Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2004, Sera ya Nishati ya Mwaka 2009, Ajenda ya Maendeleo ya Afrika 2063, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia 2030 na Hotuba za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa nyakati mbali mbali.

## 2.0 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA MIEZI TISA (JULAI – MACHI) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

***Bajeti ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024***

13. **Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuwasilisha Taarifa ya Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Muhtasari wa utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa kipindi cha miezi tisa (Julai-Machi, 2023/2024).

14. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini kupitia Idara na Taasisi zake imetekeleza Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 kupitia Programu Kuu tatu (3) na Programu Ndogo sita (6) chini ya Fungu N03. Programu Kuu hizo ni (i) Programu ya Usimamizi wa Huduma za Maji, (ii) Programu ya Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini na (iii) Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM.

***Ukusanyaji wa Mapato***

15. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Maji, Nishati na Madini ilikadiriwa kukusanya jumla ya **TZS. 15,285,400,000** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato yatokanayo na malipo ya maliasili zisizorejesheka. Hadi Machi, 2023/2024 Wizara imefanikiwa kukusanya na kuingiza katika Mfuko Mkuu wa Serikali Jumla ya **TZS. 11,713,375,451** sawa na asilimia **103** ya makadirio ya kukusanya **TZS. 11,425,498,500** ya kipindi cha tathmini.

16. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na miradi mikubwa mbalimbali ya ujenzi wa barabara nchini, jumla ya tani 3,007,442.73 za maliasili zisizorejesheka zenye thamani ya **TZS. 19,548,377,774.25** zimekosekana kutokana na tani hizo kutumika bila ya kulipwa.

**Matumizi ya kawaida**

17. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS. 126,945,949,000** kwa kazi za matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo **TZS. 1,014,100,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 2,407,600,000** kwa ajili ya mishahara, **TZS. 5,863,500,000** kwa ajili ya ruzuku ya mshahara, **TZS. 7,000,000,000** kwa ajili ya maliasili zisizorejesheka na **TZS. 110,660,749,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

18. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi, 2023/2024, Wizara imetumia **TZS. 76,507,457,419** sawa na asilimia **77** ya makadirio ya **TZS. 99,150,067,125** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara, ruzuku ya mishahara na kazi za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **TZS. 460,357,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 1,958,541,669** kwa ajili ya mishahara, **TZS. 6,417,357,108** kwa ajili ya ruzuku ya mishahara, **TZS. 63,991,754,436** kwa ajili ya miradi ya maendeleo na **TZS. 3,679,447,206** kwa ajili ya malipo ya "retention". **Kiambatisho Namba. 1** kinafafanua.

## 3.0 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA KIPINDI CHA JULAI – MACHI, 2023/2024

**19.** **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Bajeti ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, maeneo ya vipaumbele vya Wizara ya Maji, Nishati na Madini yalijumuisha:-

i. Kuimarisha upatikanaji wa huduma ya Maji, Nishati na Madini kwa kutekeleza miradi Mikubwa ya kimkakati pamoja na kufanya mapitio ya Sera, Sheria na Miongozo ya utoaji wa huduma hizo;

ii. Kuendeleza tafiti za maji pamoja na njia mbadala za kuzalisha maji safi na salama;

iii. Kutafuta Nishati Mbadala ya umeme kwa ajili ya mitambo ya kusambazia maji safi na salama ili kukidhi mahitaji ya wananchi;

iv. Kusimamia masuala ya nishati ya umeme na mafuta Zanzibar pamoja na Kushiriki katika masuala ya Nishati Kitaifa, Kikanda na Kimataifa;

v. Kuendelea na utafutaji wa Nishati Mbadala ya umeme kwa mahitaji ya Zanzibar;

vi. Kuongeza ufanisi kwa kuwapatia huduma bora wananchi;

vii. Kuongeza wateja wapya kwa kusambaza huduma ya maji na umeme katika maeneo mapya na

viii. Kuondoa changamoto katika maeneo ambayo yana uhaba wa maji na umeme mdogo.

***Sekta ya Maji (Hali ya Sekta ya Maji Nchini)***

**20.** **Mheshimiwa Spika,** maji ni rasilimali muhimu sana kwa uhai wa viumbe vyote duniani. Maendeleo yote katika jamii yanahitaji upatikanaji wa huduma bora ya maji safi na salama. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendela kuchukua jitihada za kuhakikisha wananchi wake wanapata maji safi na salama.

**21.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) inaendelea na jitihada za kuhakikisha huduma ya maji safi na salama inaimarika katika maeneo yote Unguja na Pemba. Hadi Machi, 2024,

mahitaji ya maji yamefikia lita 275,980,481 na uzalishaji lita 191,959,675 kwa siku sawa na asilimia 70 ya uzalishaji ikilinganishwa na asilimia 67 ya uzalishaji iliyofikiwa hadi Machi, 2022/2023.

22. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwepo kwa ongezeko la uzalishaji wa maji kwa siku bado kuna upungufu wa uzalishaji wa lita 84,020,806 kwa siku sawa na asilimia 30 ya mahitaji halisi. Mapungufu hayo yanasababishwa na uchakavu wa miundombinu ya maji, uvamizi wa vyanzo vya maji, mabadiliko ya tabia nchi, sambamba na kuongezeka kwa idadi ya watu, kukua kwa miji, maendeleo ya kiuchumi, kijamii, uwekezaji na kuimarika kwa sekta ya utalii.

23. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi Mijini na Vijijini inafikia zaidi ya asilimia 85 ifikapo mwaka 2025, Serikali inaendelea kujenga, kukarabati, kusambaza mitandao mipya ya maji pamoja na kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya maji.

24. **Mheshimiwa Spika,** kukamilika kwa miradi ya Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji maji na Programu ya Ahueni ya Uviko -19 kutakuwa na jumla ya visima vipya 102 vyenye uwezo wa kuzalisha lita 201,552,000 kwa siku, matangi 25 makubwa ya kuhifadhia maji lita 144,000,000, mtandao wa maji kwa masafa ya kilomita 785.9 na matarajio ya uzalishaji maji ni kufikia lita 393,511,675 kwa siku Unguja na Pemba. Hivyo, Wizara inatarajia kupunguza tatizo la upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi.

25. **Mheshimiwa Spika,** kadhalika, hali ya miundombinu na mitandao ya usambazaji maji inaendelea kuimarika licha ya kuwepo kwa changamoto ya uchakavu wa mtandao wa maji katika baadhi ya maeneo. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara inaendelea na hatua za ulazaji wa mtandao mpya wa mabomba ya maji na kubadilisha mabomba chakavu. Napenda nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wananchi wanaopata huduma ya maji safi na salama kuendelea kutoa ushirikiano kwa kuchangia huduma hiyo, ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama inaimarika zaidi. Aidha, Wizara inaendelea kufanya mazungumzo na Wawekezaji mbali mbali pamoja na Washirika wa Maendeleo kuhusiana na kuwekeza katika kuimarisha miundombinu ya maji, ili ikidhi mahitaji ya wananchi.

26. **Mheshimiwa Spika,** dhamira ya Serikali ni kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora, endelevu na ya uhakika. Hivyo, Serikali imeendelea kuimarisha Taasisi zake pamoja na kushirikisha Sekta binafsi katika uendeshaji na usimamizi wa huduma zinazotolewa. Wizara ya Maji, Nishati na Madini iliitisha zabuni ya Usimamizi na Uendeshaji wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) na imekamilisha hatua za uchambuzi kwa waliyokuwa na vigezo vya zabuni pamoja na kufanikiwa kuipata kampuni yenye uwezo wa kufanya kazi hiyo. Hatua inayoendelea ni kuanza majadiliano na kufanya uchunguzi wa kina kwa kampuni hiyo kabla ya kuingia makubaliano ya kimkataba.

27. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai-Machi, 2023/2024 Wizara imetekeleza Programu ya Usimamizi wa Huduma za Maji kwa ufanisi kama ifuatavyo: -

**Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Maji**

28. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Maendeleo ya Maji pamoja na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ambayo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS 83,768,109,000**. hadi Machi, 2023/2024 programu hii imetumia **TZS. 57,343,729,234** sawa na asilimia **86** ya makadirio ya **TZS. 66,706,141,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara, ruzuku ya mishahara na kazi za miradi ya maendeleo.

**a) Idara ya Maendeleo ya Maji**

29. **Mheshimiwa Spika,** Idara ina jukumu la kusimamia maendeleo katika sekta ya maji na kuhakikisha huduma ya maji safi na salama inapatikana kwa uhakika na endelevu. Aidha, Idara ina jukumu la kufuatilia ubora wa rasilimali maji pamoja na kufanya tafiti za maendeleo ya rasilimali maji.

30. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Afisi ya Rais Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini (PDB) iliandaa jukwaa la wataalamu kutoka Taasisi za Serikali na Washirika wa Maendeleo kwa lengo la kutafuta njia bora za kutatua changamoto katika Sekta ya Maji. Vile vile, ushirikiano huo umeimarisha ushiriki wa wadau wa maendeleo wakiwemo; GIZ, UNICEF, KfW na WaterAid kwa lengo la kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma ya maji Zanzibar.

31. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Afisi ya Rais Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utendaji Serikalini (PDB) imeandaa Mpango wa Kushirikisha Sekta Binafsi katika Sekta ya Maji kwa lengo la kuhakikisha wananchi wanapata huduma endelevu ya maji safi na salama. Mpango huo umeweza kuwapatia Kampuni binafsi ya *National Energy Center* (NEC) ya Oman kuwekeza katika mradi wa maji uliyopo Mkoa wa Kaskazini Unguja ambao ni sehemu muhimu kwa Sekta ya utalii.

32. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Uwekezaji katika Sekta ya Maji Zanzibar (*Zanzibar Water Investment Programme -ZanWIP*) kuanzia mwaka 2022 hadi 2027. Kupitia Mpango huo, Dhana nne (4) za Miradi zimeandaliwa ambazo ni; Mpango Mkuu wa Maji, Mradi wa Kuboresha Taasisi ya Maji, Mradi wa Huduma za Mkakati za Upimaji wa Maji na Mradi wa Kubadilisha Mabomba ya Zamani. Dhana hizo zimeshawasilishwa kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya kupatiwa ufadhili.

33. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Maji kwa kushirikiana na ZAWA inaendelea kuyahami maeneo ya hifadhi ya vyanzo vya maji yanayovamiwa kwa shughuli za kijamii na makaazi kwa kuweka mabango maalumu ya katazo yenye alama ya uhifadhi na umiliki wa maeneo hayo kuwa ni Mali ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ili kusitisha uvamizi, uharibifu na ufanyaji wa shughuli za aina yoyote za kiuchumi au kijamii. Jumla ya mabango 64 yamewekwa katika maeneo ya vyanzo vya maji ikiwemo Dimani, Maungani, Kidutani, Mfenesini, Dole, Mkorogo na Masingini. Utaratibu huu utaendelea katika maeneo yote ya vianzio na miundombinu ya maji kadri hali ya kifedha itakavyoruhusu.

34. **Mheshimiwa Spika,** Serikali inatumia fedha nyingi kutekeleza miradi Unguja na Pemba, ili miradi hiyo idumu ni muhimu kuwepo kwa ulinzi katika miradi pamoja na miundombinu yake. Kutokana na hujuma na tatizo la wizi linalojitokeza mara kadhaa katika visima na vituo vya maji Unguja na Pemba, Serikali imeiagiza Ofisi ya Rais, Serikali za Mitaa, Tawala za Mikoa na Idara Maalumu za SMZ kuvitumia Vikosi vyake kulinda maeneo ya vyanzo vya Maji na miundombinu, ili kuzuia na kudhibiti hujuma zinazoathiri jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwafikishia wananchi huduma ya maji safi na salama.

35. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya tathmini ya kutambua hali halisi ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama Pemba. Tathmini imebaini kuwa skimu 31 zinakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa uhakika wa huduma ya maji safi na salama. Hivyo, Wizara imeandaa Programu maalumu ya miradi yenye gharama ya **TZS. 373.9 bilioni**, ambapo utekelezaji wake utasaidia kutatua tatizo hilo. Hatua za utafutaji wa fedha hizo kupitia Wafadhili na wawekezaji kwa ajili ya utekelezaji wa programu hiyo kwa Pemba zinaendelea.

**b) Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA)**

36. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) pamoja na mambo mengine inajukumu la kuzalisha na kusambaza huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ZAWA imekadiriwa kukusanya **TZS. 10,870,491,200** kutokana na mapato yake ya ndani. Hadi Machi, 2024, **TZS. 2,746,862,440.58** sawa na asilimia **36** ya makadirio ya **TZS 7,628,784,616.00** zimepatikana kutokana na mapato ya ndani kwa kipindi cha tathmini.

37. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZAWA imeendelea kuimarisha visima vyake kwa kufunga pampu 55 (43 Unguja na 12 Pemba), ili kuimarisha hali ya uzalishaji wa maji na wananchi waendelee kunufaika na upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama. Aidha, ZAWA imeendelea kusafisha visima 61 kati ya visima 144 (Unguja 40 na Pemba 21) vilivyopangwa ndani ya kipindi cha tathmini ili kuimarisha uzalishaji na upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama.

38. **Mheshimiwa Spika,** Hadi Machi, 2023/2024 Wizara imefanikiwa kuzuia upotevu wa maji kwa kuziba jumla ya mivujo 882 iliyoripotiwa (510 Unguja na 372 Pemba). Katika kukabiliana na changamoto ya upotevu wa maji, ZAWA inaendelea kukarabati miundombinu ya maji ya zamani na kuweka mipya katika maeneo mbalimbali kupitia miradi mikubwa ya maji Unguja na Pemba. Kwa Unguja ni Maungani, Dimani, Mwera, Donge-Tumbatu na kwa Pemba maeneo ya Makangale, Micheweni, Tungamaa, Mapofu-Wingwi na Mwambe. Hatua hii itapelekea kupunguza upotevu wa maji kwa kiasi kikubwa.

39. **Mheshimiwa Spika,** ZAWA imeendelea kusajili na kuwaunganisha wateja na huduma ya maji safi na salama mijini na vijijini. Kwa kipindi cha Julai - Machi 2024, jumla ya wateja wapya 2,785 (1,593 Unguja na 1,192 Pemba) kati ya wateja 6,000 waliokadiriwa sawa na asilimia 46 wamesajiliwa na kuunganishwa na huduma ya maji. Hatua hii imeonesha kupungua kwa wateja ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambapo wateja 3,664 (2,254 Unguja na 1,410 Pemba) waliunganishwa na huduma ya maji. Upatikanaji wa wateja wapya ambao wamefungiwa mita za malipo utarahisisha upatikanaji wa huduma ya uhakika kupitia malipo yatakayosaidia gharama za uendeshaji.

40. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZAWA imeandaa na kurusha hewani Makala ya Miaka Mitatu ya Mafanikio ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Awamu ya Nane. Aidha, vipindi vitano (5) maalumu vya TV vimeandaliwa na kurushwa hewani kupitia ZBC-TV vilivyohusu miradi, kazi za uimarishaji na upatikanaji wa huduma za maji katika maeneo ya Unguja na Pemba, uendelezaji wa miradi kwa kushajiisha ulipaji wa huduma ya maji na utunzaji wa miundombinu na vyanzo vya maji.

41. **Mheshimiwa Spika,** vile vile, mikutano ya uhamasishaji imeendelea kufanyika katika maeneo ya Unguja na Pemba iliyohusiana na kutunza na kulipia huduma ya maji. Mikutano hii imefanyika Unguja katika maeneo ya Chaani, Masingini na Kendwa na kwa Pemba katika maeneo ya Kiwani, Nanguji, Chwale, Madenjani, Pandani na Kengeja. Hatua hii imesaidia kuongeza uelewa juu ya usimamizi endelevu wa rasilimali maji na wananchi kuweza kufanya matumizi bora ya maji, kuchangia huduma ya maji pamoja na kutunza miundombinu ya maji na vyanzo vyake.

42. **Mheshimiwa Spika,** ZAWA imeendelea kupokea malalamiko ya wananchi kuhusu changamoto za upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kupitia mfumo wa Sema Na Rais (SNR) na kuyafanyia kazi. Kwa kipindi cha Julai – Machi, 2023/2024 jumla ya malalamiko 146 yameripotiwa ambapo 81 yametatuliwa na 65 yanaendelea kutafutiwa ufumbuzi. Malalamiko hayo yalihusiana na kuchelewa kulipwa fidia ya vipando na mali zilizoathirika na ujenzi wa miradi ya maji Unguja, pamoja na upungufu na ukosefu wa huduma za maji safi na salama katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

*Sekta ya Nishati (Hali ya Sekta ya Nishati Nchini)*

43. **Mheshimiwa Spika,** Mwaka 1980 Visiwa vya Zanzibar vilianza kutumia umeme wa gridi ya Taifa. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iligharamia kuweka waya wa kwanza wa baharini (Submarine Cable) kutoka Ras-Kiromoni hadi Ras-Fumba wenye uwezo wa Megawati 45. Waya ambao uliendelea kutumika hadi mwaka 2009 baada ya kuzidiwa kutokana na mahitaji ya wakati huo yaliyokuwa Megawati 52. Hali hiyo ilipelekea kuwa na mgao wa umeme hadi mwaka 2013 ulipomalizika mradi wa ulazaji wa waya mwengine wa baharini wenye uwezo wa Megawati 100.

44. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kukamilika kwa mradi huo Aprili, 2013 Shirika la Umeme lilisitisha matumizi ya waya wa zamani kutokana na waya mpya kutosheleza mahitaji ya umeme kwa wastani wa Megawati 52 katika kipindi hicho. Aidha, kwa upande wa Pemba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Norway ilifanikisha mradi wa uwekaji waya wa baharini wenye uwezo wa Megawati 20 uliounganishwa kutoka Tanga hadi Pemba ambao unaendelea kutumika.

45. **Mheshimiwa Spika,** matumizi ya umeme yaliendelea kupanda kutokana na kasi ya maendeleo nchini ambapo matumizi ya juu yalifikia Megawati 90.3 kupitia laini ya 100MW na 29MW kupitia laini ya 45MW kwa Unguja na Pemba Megawati 13 kupitia laini ya 20MW. Hali hiyo ilipelekea Shirika la Umeme Zanzibar kuendelea kutumia nyaya zote mbili kuanzia tarehe 23/11/2022.

46. **Mheshimiwa Spika,** tumekuwa tukishuhudia kukatika kwa umeme mara kwa mara. Sababu za kukatika kwa umeme zimegawika katika makundi mawili (2) ambayo ni; kukatika kwa umeme kwa kutokupanga (*Unplanned outage*) na kukatika kwa umeme kwa kupanga (*Planned outage*). Hali ambayo inapelekea kuathiri utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii.

47. **Mheshimiwa Spika,** kukatika kwa umeme kwa kutokupanga kunasababishwa na mambo yafuatayo:-

   i. **Kushuka kwa kiwango cha voltage kutoka katika gridi ya taifa:** Kisiwa cha Unguja kwa kawaida kinapaswa kupokea kiwango cha kilovolti 132 kutoka gridi ya taifa lakini katika hali isiyo ya kawaida kiwango hicho kinashuka hadi kufikia kilovolti 118 kunakotokana na matumizi makubwa ya umeme katika maeneo ya viwanda Tegeta na

Kunduchi hali inayopelekea kuzimwa kwa baadhi ya laini za umeme, ili kuepusha kuzimwa laini zote;

ii. **Kuzidiwa kwa mtandao wa kusambazia umeme:** Zanzibar inaendelea kushuhudia ukuaji wa kasi wa maendeleo unaotokana na ujenzi wa miundombinu ya miradi ya kimkakati katika sekta mbali mbali ikiwemo; utalii, afya na elimu. Hata hivyo, ukuaji huo hauendi sambamba na maboresho ya miundombinu mipya ya umeme, ikichangiwa na miundombinu chakavu iliyopo ambayo inazorotesha ufanisi wa upatikanaji wa huduma hiyo;

iii. **Athari za Kimazingira:** laini nyingi za kusafirishia na kusambazia umeme zimezungukwa na mazingira hatarishi ikiwemo kupitiwa na miti mikubwa, hali inayopelekea baadhi ya wakati kukosekana kwa huduma ya umeme kwa laini hizo; na

iv. **Ujenzi wa Miundombinu ya Barabara:** Ujenzi wa barabara umekuwa ukichangia kukatika kwa umeme kutokana na kuathiri miundombinu ya usambazaji wa umeme iliyopo juu na chini ya ardhi wakati wa utekelezaji wa miradi.

**48.** **Mheshimiwa Spika,** kukatika kwa umeme kwa kupanga kunasababishwa na unganishaji wateja wenye mahitaji makubwa ya umeme mfano mahoteli yenye transformer zao binafsi. Matengenezo ya kawaida ya njia za kusambazia na kugawia umeme ambayo hutolewa tangazo kupitia vyombo vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii.

## Mikakati Inayoendelea Kutatua Changamoto za Sekta ya Nishati

**49.** **Mheshimiwa Spika,** jitihada mbali mbali zinaendelea kuchukuliwa katika kukabiliana na changamoto ya umeme ikiwa pamoja na changamoto ya kukatika kwa umeme mara kwa mara. Jitihada hizo ikiwemo kutafuta suluhisho la muda mrefu ambapo Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Mabadiliko ya Sekta ya Nishati na Ufikiwaji wa Huduma ya Nishati kwa Wananchi (ZESTA). Mradi huo utajenga laini kubwa ya kusafirishia umeme yenye Mkondo wa Kilovolti 132 kutoka Welezo kuelekea Makunduchi na Matemwe pamoja na vituo vya kupozea umeme katika maeneo hayo.

50. **Mheshimiwa Spika,** kwa hatua za muda mfupi na wa kati Shirika la Umeme Zanzibar limejenga laini kubwa tatu (3) kwa ajili ya kuweka uwiano na kuondoa tatizo la kukatika umeme katika maeneo ya Nungwi, Matemwe, Kiembe-samaki na Chukwani. Laini hizo zimejengwa, ili kuzipunguzia mzigo laini za Kaskazini Mpya, Kaskazini Kongwe pamoja na laini ya Mazizini.

51. **Mheshimiwa Spika,** jitihada nyengine iliyochukuliwa ni kuajiri Kampuni ya *"Novavis International"* kutoka Marekani kwa ajili ya kutatua changamoto ya umeme mdogo katika maeneo ya Unguja na Pemba. Kampuni hiyo inaendelea na kazi ya uwekaji wa nguzo za zege pamoja na sakafu zake kwa ajili ya kufunga vifaa maalumu vya kuongeza nguvu ya umeme katika maeneo mbali mbali yakiwemo Paje, Jambiani, Michamvi, Nungwi, Kiwengwa, Matemwe, Uroa na Chwaka. Mradi huu kwa hatua ya mwanzo utaanza majaribio Septemba, 2024.

52. **Mheshimiwa Spika,** katika kukabiliana na changamoto ya kuzidiwa kwa nyaya zinazotumika kuingiza umeme Zanzibar kutoka Tanzania Bara, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia TANESCO na ZECO zitatekeleza mradi wa kulaza waya mwengine wa baharini wenye uwezo wa Megawati 200 kupitia laini ya 220kV kwa Unguja na Megawati 100 kupitia laini ya 132kV kwa Pemba. Vile vile, kubadilisha laini zote za kusafirishia umeme za mkondo wa 11kV na kuweka laini ya mkondo wa 33kV katika maeneo yote ya Pemba. Hatua iliyofikiwa Mshauri Elekezi anaendelea na kazi ya Upembuzi yakinifu kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Mradi huu utaimarisha upatikanaji wa huduma ya umeme wa uhakika.

53. **Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia ZECO inaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua kupitia Kampuni ya *"Generation Capital Limited"* ambayo kwa awamu ya kwanza itazalisha Megawati 30 za umeme Unguja katika eneo la Bambi na Pemba kupitia Kampuni ya ESR itazalisha Megawati 15 katika eneo la Micheweni. Miradi hiyo inaendelea kutekelezwa na inatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa 2025. Vile vile, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa ZESTA ambao utazalisha Megawati 18 kwa kutumia nishati ya jua pamoja na mfumo wa uhifadhi wa umeme wenye uwezo wa Megawati 40 kwa saa. Aidha, Wizara imetangaza zabuni ya kutafuta kampuni zenye uwezo wa kuzalisha Megawati 50 za gesi au nishati inayofanana nayo na

Megawati 5 za umeme unaotokana na takataka. Hatua hii itahakikisha upatikanaji wa chanzo cha uzalishaji wa umeme wa uhakika.

54. **Mheshimiwa Spika,** dhamira ya Serikali ni kuwapatia wananchi huduma bora, endelevu na za uhakika, katika kutekeleza azma hiyo, Serikali inaendelea kuimarisha Taasisi zake katika uendeshaji na usimamizi wa huduma zinazotolewa kwa wananchi. Hivyo, Wizara ya Maji, Nishati na Madini iliitisha zabuni ya Usimamizi na Uendeshaji wa ZECO kwa Kampuni mbali mbali na imekamilisha hatua za uchambuzi kwa waliyokuwa na vigezo na hatimae kuipata Kampuni yenye uwezo wa kuifanya kazi hiyo. Hata hivyo, majadiliano na uchunguzi wa kina kwa kampuni hiyo yanaendelea kabla ya kuingia makubaliano ya kimkataba. Matarajio ya Serikali kwa upatikanaji wa kampuni hiyo ni kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za umeme zenye tija kwa wananchi na kuongeza kasi ya ukuaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi.

55. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai-Machi, 2023/2024, Programu kuu ya Usimamizi wa Huduma ya Nishati na Madini ilitekeleza Programu zake kama ifuatavyo:-

**Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma ya Nishati na Madini**

56. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa na Idara ya Nishati na Madini, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) pamoja na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) ambayo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ilikadiriwa kutumia jumla ya **TZS 41,028,270,000**. Hadi Machi 2023/2024 programu hii imetumia **TZS. 17,570,317,805** sawa na asilimia **57** ya makadirio ya **TZS. 30,807,279,500** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara, miradi ya maendeleo na malipo ya "retention".

**a) Idara ya Nishati na Madini**

57. **Mheshimiwa Spika,** Idara hii ina jukumu la kuratibu masuala ya nishati ikiwemo nishati mbadala, nishati ya kisasa, mafuta, gesi asilia, umeme pamoja na kutoa elimu ya matumizi sahihi ya nishati kwa jamii. Idara inatekeleza majukumu yake  na kupata mafanikio mbalimbali.

58. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kuhakikisha Zanzibar inapata vyanzo vyake vya ndani vya uzalishaji umeme pamoja na kuwepo kwa miundombinu imara ya kusafirishia na kusambaza umeme. Kwa kufanikisha hilo, Wizara

ilisaini MoU na Kampuni ya Grid X Africa tarehe 30/08/2023 kwa lengo la kuwekeza katika nishati ya jua kwa Megawati 20 kwa saa  na uhifadhi wa betri kwa Megawati 20 kwa saa Mkataba huo utawezesha Upembuzi Yakinifu wa uwezekano wa kutekelezeka kwa mradi huo katika nyanja ya kifedha na kiufundi. Pia, Wizara imeingia mkataba na Kampuni ya *"Sany & Aseel Oilfield Services"* kwa uzalishaji wa umeme kupitia upepo wenye jumla ya Megawati 100. Majadiliano ya mkataba wa mauziano "PPA" yanaendelea na utekelezaji utaanza baada ya kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu wa mradi huo.

**59.** **Mheshimiwa Spika,** kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya umeme na kukua kwa uchumi, Wizara ya Maji, Nishati na Madini imeandaa Mpango Mkuu wa Umeme wa mwaka 2023-2050 *(Zanzibar Power Master Plan* 2023/2050)  ambao utakuwa ni Dira ya Taifa katika uwekezaji wa Sekta ya Nishati Zanzibar.

**60.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha Gridi na kuondoa changamoto ya umeme mdogo na kukatika mara kwa mara, Wizara imeingia Mkataba tarehe 25/07/2023 na Kampuni ya Novavis kutoka Marekani kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo. Mkataba huo unatekelezwa kwa muda wa miezi 18 kuanzia tarehe uliyosainiwa, ambapo kampuni inaendelea na kazi ya utekelezaji.

**61.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha wananchi wanatumia nishati safi ya kisasa yenye kutunza mazingira, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Taifa la Madini (STAMICO) imesaini Hati ya Makubaliano ya ushirikiano ambayo imeanza utekelezaji wake. Miongoni mwa mafanikio yaliyopatikana ni kuratibu uingizwaji wa mkaa safi na salama *"Rafiki Briquettes"* utokanao na Mkaa wa mawe kwa matumizi ya kupikia kutoka Tanzania Bara, ambao umesarifiwa kuondoa sumu zote chafuzi kwa mazingira.

**62.** **Mheshimiwa Spika,** kupitia ushirikiano baina ya Wizara na STAMICO, watendaji watano (5) walipatiwa mafunzo ya uzalishaji wa Mkaa safi na salama *"Rafiki Briquttes"*. Mafunzo hayo yamewaongezea uelewa na kuwahamasisha wafanyabiashara na wananchi juu ya umuhimu wa matumizi ya mkaa safi na salama na kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na ukataji miti holela. Aidha, Wizara inaendelea na mazungumzo ya kuwaomba STAMICO kufunga mtambo wa kuzalisha mkaa huo Zanzibar, ili kurahisisha upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa wananchi kwa gharama nafuu.

63. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeshiriki kikao cha wadau na kutoa maoni juu ya mapendekezo ya mradi wa majiko sanifu Zanzibar yanayotumia *"Biofuel"* inayozalishwa kwa mabaki yanayotokana na utengenezaji wa sukari. Kikao hicho kiliandaliwa na Taasisi ya Umoja wa Kimataifa inayohusiana na Maendeleo ya Viwanda ambayo ndiyo inayosimamia mradi. Mradi huu umepangwa kutekelezwa kwa pande zote mbili za Muungano (Tanzania Bara na Zanzibar), ikiambatana na utoaji elimu kwa wananchi.

64. **Mheshimiwa Spika,** katika hatua nyingine, Wizara imeshiriki warsha ya kuandaa mapendekezo ya miradi ya kupunguza uharibifu wa mazingira kupitia Programu ya Maendeleo ya Umoja wa Mataifa (UNDP) kwa lengo la kuandaa mapendekezo ya kuomba fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya mabadiliko ya tabianchi na kupunguza utoaji wa gesi chafu. Aidha, mapendekezo ya mradi wa kuingiza magari ya umeme *"e-vehicle"* pamoja na kuweka vituo vya kujazia chaji vitakavyotumia umeme wa jua ilipewa kipaumbele kutayarishwa.

65. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya majadiliano na kampuni 12 za uwekezaji wa nishati ya umeme wa kutumia jua, upepo, gesi, maji na taka ambapo iliainisha vipaumbele vyake juu ya uzalishaji wa umeme na kuwatembeza baadhi ya Wawekezaji katika maeneo ya Makunduchi, Bambi na Matemwe yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji wa Nishati ya Umeme, ili waweze kuendelea na hatua za Upembuzi Yakinifu juu ya uwezekano wa kuzalisha umeme wa Upepo na Jua katika maeneo hayo.

66. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ilifanya ukaguzi wa Hoteli katika Ukanda wa Kaskazini Unguja katika Shehia za Nungwi, Kendwa na Kiwengwa, ili kutathmini changamoto za upatikanaji wa huduma bora ya umeme. Hoteli 15 zilikaguliwa na kubaini changamoto mbali mbali ikiwemo kukatika kwa umeme mara kwa mara, hali inayowapelekea wamiliki wa hoteli kutumia majenereta ya dizeli na kuongeza gharama kwa watumiaji. Pia, uwepo wa umeme mdogo unaosababisha vifaa muhimu kama pampu za maji, vipoza hewa (AC) na kompresa za vyumba vya baridi (cold rooms) kuungua, hivyo kulazimika kununua stabiliza za gharama kubwa, ili kudhibiti upungufu wa umeme.

67. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuchukua jitihada za kukabiliana na changamoto hizo ikiwa pamoja na kutekeleza miradi ya maendeleo. Miongoni mwa miradi hiyo ni mradi wa ZESTA ambao utazalisha umeme

wa jua wenye uwezo wa Megawati 18 pamoja na ujenzi wa laini mpya zenye mkondo wa 132kV kuelekea Kaskazini na Kusini Unguja. Utekelezaji wa mradi huo, utasaidia kutatua changamoto ya umeme mdogo pamoja na kufanyia marekebisho miundombinu ya umeme.

**b) Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)**

68. **Mheshimiwa Spika,** Shirika linaendelea na utoaji wa huduma ya umeme kwa wananchi wa Zanzibar, ambapo hadi Machi, 2024 jumla ya uniti 457,190,425.20 kWh zimeuzwa kati ya 445,079,031 kWh zilizopangwa sawa na asilimia 103 ya mauzo na kupelekea mauzo ya jumla ya **TZS. 114,924,932,050.10** ambayo hayajajumuisha tozo ya Ongezeko la Thamani (VAT).

69. **Mheshimiwa Spika,** mahitaji ya umeme yameendelea kukua kwa wastani wa Megawati 21.3 baina ya mwaka 2021 hadi 2024. Mahitaji ya juu ya umeme *"Peak demand"* kwa Unguja yamefikia Megawati 121 (matumizi katika waya wa Megawati 100 yamefikia Megawati 90.8 na waya wa megawati 45 yamefikia Megawati 30) sawa na asilimia 83 ya uwezo wa nyaya mbili zilizopo yaliyofikiwa tarehe 13 Machi 2024. Aidha, kwa upande wa Pemba mahitaji ya juu ya umeme ni Megawati 13.50 sawa na asilimia 67.5 ya uwezo wa waya unaotumika hadi sasa wa Megawati 20.

70. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO imeendelea kuimarisha Gridi ya Taifa kwa kuongeza mtandao wa usambazaji umeme kwa kiwango cha 33kV na 11kV. Hadi Machi, 2024 mtandao wa kusafirisha umeme umefikia jumla ya kilomita 3,398.10 sawa na ongezeko la asilimia 106 ikilinganishwa na kilomita 1,645 zilizofikiwa Machi, 2023.

71. **Mheshimiwa Spika,** aidha, Wizara kupitia ZECO imefanikiwa kujenga njia za umeme mdogo wa msongo wa 400V wenye urefu wa kilomita 94.80 sawa na asilimia 65 ya kilomita 144 iliyopangwa kujengwa. Kuna ongezeko la asilimia 13 ikilinganishwa na kilomita 83.28 zilizofikiwa katika kipindi cha miezi tisa ya Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ongezeko hili limetokana na mahitaji ya ujenzi wa njia kuu na idadi kubwa ya wateja wanaoungiwa umeme.

72. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO inaendelea kusambaza na kuuza umeme kwa wananchi. Hadi Machi, 2023/2024, ZECO imekusanya **TZS. 132.75 Bilioni,** sawa na asilimia **99** ya makadirio ya kukusanya **TZS. 134.19 Bilioni.** Makusanyo hayo yametokana na mauzo ya umeme na

mapato mengineyo, ambapo jumla ya **TZS. 121.8 Bilioni** (mauzo ya umeme) na **TZS. 10.95 Bilioni** (mapato mengineyo). Pamoja na mafanikio hayo, Shirika linakabiliwa na changamoto ya kutolipwa madeni kutoka Taasisi za Serikali na Binafsi SMZ na SMT. Jumla ya **TZS. 63,805,980,321.3**4 ya deni linalodai, ikiwa ni punguzo la asilimia **2** ya deni kwa kipindi cha Julai-Machi 2022/2023 lililokuwa **TZS. 65,091,321,485.93.**

**73. Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto ya deni hilo, Serikali imechukua hatua za kutoa **TZS. 1.5 Bilioni** kila mwezi kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina ikiwa ni hatua ya Serikali ya kupunguza deni ambalo Shirika linaidai ZAWA. Hadi Machi, 2024 **TZS. 4.5 Bilioni** zimelipwa. Hatua hii inaashiria nia ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kushughulikia kwa vitendo changamoto za kiuchumi zinazoikabili nchi.

**74. Mheshimiwa Spika,** hadi Machi, 2023/2024 ZECO imebadilisha jumla ya nguzo mbovu 1,661 (1,344 Unguja na 317 Pemba) pamoja na kuimarisha upatikanaji wa umeme katika maeneo 36 (Unguja 32 na Pemba manne (4)), ambayo awali yalikuwa yakikabiliwa na changamoto ya umeme mdogo. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 109 ya mpango uliyowekwa katika maeneo 33 (Unguja 27 na Pemba sita (6)) **Kiambatisho Namba 2** kinahusika.

**75. Mheshimiwa Spika,** ZECO imewaunganishia umeme wateja wapya 25,280 (21,017 Unguja na 4,263 Pemba) sawa na asilimia 88 ya wateja 28,800 (Unguja 23,400 na Pemba 5,400) waliyoomba kuunganishiwa umeme. Pia, ZECO imekagua jumla ya transfoma 905 (Unguja 611 na Pemba 294) sawa na asilimia 73.0 ya transfoma 1,239 (Unguja 900 na Pemba 339). Kati ya transfoma 905 zilizokaguliwa, jumla ya transfoma 51 kwa Unguja na saba (7) Pemba zilibainika kuwa na hitilafu na kufanyiwa masawazisho. Ukaguzi huo umesaidia kuondoa changamoto na kuimarisha upatikanaji wa huduma ya umeme.

**76. Mheshimiwa Spika,** ZECO ilipanga kusambaza huduma ya umeme katika vijiji 45 (Unguja 27 na Pemba 18) na kufanikiwa kupeleka huduma ya umeme katika vijiji 45 vilivyopangwa kufikishiwa huduma hiyo. Aidha, upotevu wa umeme umepungua kwa asilimia 0.73 kutoka asilimia 16.0 hadi asilimia 15.27 kwa mwaka 2023/2024 kupitia jitihada za ukaguzi wa wateja, kubadilisha mita mbovu na kufunga mita zinazojisoma wenyewe (AMR) kwa wateja wakubwa.

### c) Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)

**77. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) ina jukumu la kudhibiti huduma za maji na nishati, ili huduma hizo zipatikane kwa kiwango bora na chenye uhakika. Wizara inaendelea kudhibiti huduma za maji na nishati kwa matumizi ya kiuchumi na kijamii.

**78. Mheshimiwa Spika,** hadi Machi, 2023/2024, ZURA imefanikiwa kukusanya jumla ya **TZS. 18,772,632,023.5** sawa na asilimia **107** ya makadirio ya **TZS. 17,599,256,023.5.** Makusanyo hayo yanatokana na tozo za mafuta na mapato mengineyo (leseni, adhabu na ukodishaji wa ukumbi wa mikutano). Ikilinganishwa na kipindi cha tathmini Julai-Machi 2022/2023 kuna ongezeko la **asilimia 18** ya makusanyo halisi yaliyokuwa **TZS.15,947,436,329.** Ongezeko hili limetokana na kasi ya uingizaji wa mafuta nchini uliochochea shughuli za kimaendeleo na kiuchumi.

**79. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa matumizi, hadi Machi, 2023/2024, ZURA ilitumia jumla ya **TZS. 13,356,511,670.75** sawa na asilimia **67** ya makadirio ya matumizi ya **TZS. 19,952,360,038** kwa kipindi cha tathmini. Kati ya fedha hizo **TZS. 6,638,590,106.02** zilitumika kwa kazi ya kawaida, **TZS. 117,397,199.05** kwa kazi za miradi ya maendeleo na **TZS. 6,300,000,000** ni mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

**80. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZURA imeimarisha nyenzo muhimu za udhibiti ikiwa pamoja na kuandaa Kanuni za Ubora wa Maji, Kanuni za Usimamizi wa Mikataba ya Ununuzi wa Umeme, Rasimu ya Awali ya Mikataba ya Utendaji Kazi ya ZECO na ZAWA pamoja na Rasimu ya Kanuni ya Ubora wa Huduma za Umeme. Hatua hii imeongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Taasisi na upatikanaji wa huduma bora kwa wananchi.

**81. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZURA imeandaa Muongozo wa Ujenzi wa Bohari ya kujazia Gesi ya kupikia ambao unasaidia usimamizi katika Sekta ya Mafuta na Gesi ili kuwapatia huduma bora wananchi. Aidha, ZURA imeingia Mikataba miwili ya Usimamizi wa Uingizaji wa Mafuta kwa Jumla na mletaji mafuta pamoja na Mkataba wa Ununuzi wa Mafuta baina ya kampuni ya OMC na ZURA. Miongozo hii imesaidia

usimamizi mzuri wa Sekta ya Mafuta na Gesi katika kuwapatia huduma bora wananchi.

**82.** **Mheshimiwa Spika,** ZURA imekagua ubora wa maji wa visima 59 kati ya 87 vinavyosambaza maji kwa watumiaji katika Wilaya sita (6) ambazo ni; Wilaya ya Kusini visima 10, Wilaya ya Kati visima nane (8), Wilaya ya Magharibi "A" visima tisa (9), Wilaya ya Magharibi 'B' visima 14, Wilaya ya Kaskazini 'A' visima sita (6) na Wilaya ya Kaskazini 'B' visima 12. Ukaguzi huo umebaini ubora wa maji wa visima hivyo vimekidhi viwango elekezi vya Shirika la Afya Duniani (WHO) na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kwa vigezo vilivyopimwa.

**83.** **Mheshimiwa Spika,** ukaguzi wa miundombinu ya kusambaza umeme umefanyika kwa Mkoa wa Kaskazini, Kusini na Wilaya ya Magharibi "B" - Mkoa wa Mjini Magharibi-Unguja katika maeneo ya njia za kusambaza umeme, ili kutambua hali halisi ya huduma ya umeme. Katika ukaguzi huo, vituo 96 vilikaguliwa (58 vya Kaskazini Mpya na Kongwe na 38 vya Bambi, Fumba, Kusini Mpya na Kongwe).

**84.** **Mheshimiwa Spika,** ukaguzi huo umebaini kuungua kwa vizibiti vya transfoma katika sehemu ya kupokelea umeme mkubwa kulikosababishwa kwa kuunganishwa waya moja kwa moja bila ya kutumia vifaa maalumu vya kulinda transfoma "*drop out fuse*" katika maeneo ya Mbweni Karume, Barabara ya Buyu, Dimani Bondeni (ZAWA) na Bweleo kwa Mkorea. Aidha, maeneo mengine ni Mtule AMKOS Saccos, Mpilipilini, Paje Polisi, Paje Njiani, Bwejuu Skuli, Michamvi Pigwe, Uroa Dikoni, Pongwe mwisho na Hanyegwa Magereza. Kasoro hizo zishafanyiwa kazi na ZECO.

**85.** **Mheshimiwa Spika,** aidha, ukaguzi wa usalama wa nyaya za transfoma 38 ulifanyika. Kati ya transfoma hizo 13 zimebainika kuwa na mfumo wa kiusalama wa nyaya zilizounganishwa pamoja *"Lighting Arrester and Earth"* katika kituo cha kusambaza umeme Nungwi njia ya Mnarani. Wizara kupitia ZECO, imechukua hatua za kukabiliana na changamoto hii, ili kuhakikisha usalama kwa wananchi na imebaini baadhi ya nguzo za transfoma zinahitaji kubadilishwa ikiwemo Kituo cha kusambaza umeme Tomondo Changu, Fumba Kijijini na Nyamanzi njia ya Fumba. Nguzo zote tayari zimebadilishwa na wananchi wanaendelea kupata huduma ya umeme.

**86. Mheshimiwa Spika,** ukaguzi katika miundombinu ya ufungaji wa waya *"Transformer Dressing"* katika vituo vya Chukwani kituo cha Daladala, Dimani Bondeni (ZAWA) na Bwefumu Skuli umebaini haviko katika hali nzuri. Aidha, baadhi ya vituo vya kusambaza umeme vinatumia njia moja ya kusambaza umeme badala ya kutumia njia tatu, hivyo husababisha umeme mdogo kwa watumiaji.

**87. Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, ukaguzi umebaini nguzo zilizoekewa transfoma katika vituo vya Hanyegwa Magereza na Hanyegwa kiwanda cha matofali ni mbovu na Miundombinu ya transfoma *"transformer dressing"* katika vituo vya Paje Polisi, Bwejuu Skuli, Michamvi Pingwe, Michamvi Kae Skuli, Hanyegwa P/S, Ndijani Skuli, Marumbi na Uroa haipo katika mazingira mazuri. Vile vile, Waya za usalama wa transfoma zimekatwa katika vituo vya Mpilipilini, Mtule AMKOS Saccos na Michamvi Pingwe na Kituo cha Mwera kina miundombinu duni ya transfoma. Changamoto hizi zinaendelea kufanyiwa kazi.

**88. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZURA imefanya ukaguzi maalumu katika miundombinu ya kusambaza umeme kwa vituo vitano (5) ambavyo ni Fuoni Meli tano, Fuoni kwa Amina Abduli, Chaani Masingini, M/kwe C (Masjid), Tunguu (Haji Omar) na kubainika kasoro ikiwa pamoja na "Fuse" za umeme mdogo (LV) zimefungwa moja kwa moja, Waya za kusambaza umeme katika transfoma haziridhishi *"Metal earth"* na *"lighting arrester earth"* zimeunganishwa pamoja na nguzo inayoleta umeme mkubwa karibu na transfoma imeanza kuoza, kukosekana kwa uzio na alama ya tahadhari katika eneo la trasfoma, Transfoma na Fuse za umeme mkubwa (HT) zimefungwa moja kwa moja.

**89. Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto zilizobainika, ZURA inaendelea kutoa miongozo na maelekezo ya kitaalamu kwa kushirikiana na wataalamu wa ZECO katika kurekebisha dosari zilizobainika, ili kuimarisha upatikanaji wa huduma ya umeme kwa wananchi.

**90. Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa udhibiti wa huduma za mafuta, Wizara kupitia ZURA ilikadiria kuingiza mafuta lita 170,796,637 mafuta yaliyoingizwa nchini yalifikia lita 185,525,066 na yaliyotumiwa yalifikia lita 184,289,415.00 ukilinganisha na kipindi cha Julai - Machi, 2022/23, mafuta yaliyokadiriwa kuingia nchini yalifikia lita 135,652,174 na yaliyoingizwa yalifikia lita 165,955,023. Mafuta yaliyoingizwa na

kampuni ya GAPCO ni lita 51,689,200, PUMA lita 44,635,367, UGL lita 49,581,807 na ZPL lita 39,618,692. **Kiambatisho Namba.3 kinahusika.**

**91. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZURA imekagua Bohari tano (5) (Unguja nne (4) na Pemba moja (1)). Aidha, ukaguzi wa vituo vya mafuta umefanyika ambapo vituo 108 vilikaguliwa (Unguja 89 na Pemba 19). Vituo 12 kati ya 108 havikukidhi matakwa ya Kanuni ya Usimamizi wa Vituo vya mafuta ya mwaka 2022. Hii imesababishwa na kukosekana kipaa na maeneo madogo. Hivyo wamiliki wa Vituo wamepewa muda wa kufanya marekebisho kabla ya kupatiwa leseni za biashara. Vituo hivyo kwa Unguja ni Ngwanda Petrol Station, Malawi Petrol Station, Kijichi Petrol Station, Coral Reef (Nungwi) na Kiwengwa Petrol Station na kwa Pemba ni Kengeja Petrol Station, Bakar Petroleum Station, Chake Petrol Station, Sharif Petrol Station, Tibirinzi Service Station, Chasasa Service Station na Wingwi Petrol Station.

**92. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupita ZURA imeendelea kufanya ukaguzi wa maeneo mapya 16 yanayotarajiwa kujengwa vituo vipya vya mafuta. Kati ya maeneo hayo, maeneo 14 yametakiwa kukamilisha taratibu za maombi, ili kupatiwa vibali vya ujenzi. Maeneo yaliyoruhusiwa kuendelea na ujenzi ni Fuoni Kibondeni, Kizimkazi Dimbani, Chuini, Ndagaa, Kitogani, Paje Mpilipilini, Bweleo, Hanyegwa, Cheju, Ukongoroni, Mahonda Mtomchanga, Mkanyageni, Paje Mtule (Salah) na Paje Mtule (Osward).

**93. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZURA iliratibu ukaguzi wa uwekaji alama katika mafuta yanayoingizwa nchini, ili kupunguza udanganyifu. Jumla ya lita 62,397,253 za mafuta ya Petroli na Dizeli zimewekewa alama ya T1. Mafuta ya Taa yaliyowekewa alama ya T2 ni lita 823,950. Utaratibu wa uwekaji alama ulisitishwa tarehe 31/10/2023 baada ya Mamlaka kumaliza mkataba na kampuni ya uwekaji wa alama hizo. Kadhalika, ukaguzi wa bei za mafuta ulifanyika, ili kujiridhisha na bei halisi za mafuta zilizotangazwa. Ukaguzi umebaini vituo vyote vimeweka bei elekezi zilizotangazwa na Mamlaka. Bei hizo zinaonekana katika **Kiambatisho Namba. 4.**

**94. Mheshimiwa Spika,** ZURA imeendelea kudhibiti na kutoa leseni kwa bidhaa ya gesi kwa waingizaji na wasambazaji wa bidhaa hiyo inayotumika majumbani (LPG) ambao ni ORYX Gas Tanzania Ltd, Lake Gas Ltd, Taifa Gas Tanzania Ltd, Al Nabahan Gas Supply (O-Gas) na M GAS. Kwa

kipindi cha Julai-Machi, 2024 kiasi cha gesi iliyoingizwa na kutumika Zanzibar inaonekana katika **Kiambatisho Namba. 5.**

**95. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZURA imeendelea kusimamia upangaji wa bei za gesi kupitia kampuni zinazoingiza gesi kwa ujumla kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo.

***Jadweli: linaonesha taarifa za ujazo na bei za gesi kwa kipindi cha Julai -Machi 2024***

| KILOGRAMU (KG) | BEI MWEZI (JULAI-MACHI) |
|---|---|
| 3 | 12,000-13,000 |
| 6 | 20,000-25,000 |
| 15 | 50,000-60,000 |
| 38 | 120,000-150,000 |

***Chanzo: ZURA 2024***

**96. Mheshimiwa Spika,** ZURA imeendelea kuwapatia mafunzo wafanyakazi 25 kuhusu gharama ya gesi ya majumbani na mafunzo ya kutengeneza Bei za Maji na Umeme kupitia wataalamu kutoka EWURA. Aidha, wameratibu mafunzo kwa Wajumbe wa Bodi Mkoani Morogoro kuhusu masuala ya Fedha na Uhasibu. Zaidi ya hayo, walifanya ziara katika Mamlaka ya Maji safi na Maji taka - Arusha, ambayo yameimarisha utendaji na ufanisi wa majukumu yao ya kazi.

**97. Mheshimiwa Spika,** ZURA imeongeza elimu kwa jamii kupitia vyombo vya habari na makongamano ya kijamii kwa lengo la kujitangaza, kueleweka na kutatua malalamiko ya watumiaji wa huduma za Maji na Nishati Zanzibar. Shughuli za elimu kwa jamii zilijumuisha vipindi mbali mbali vya TV kupitia ZBC TV na Redio, Redio Jamii Mkoani na Micheweni. **Kiambatisho Namba 6. kinahusika.**

**98. Mheshimiwa Spika,** ZURA, imeendelea kutoa misaada katika matukio mbali mbali ya jamii ikiwa pamoja na kununua vitendea kazi katika Skuli ya Sekondari Ali Hassan Mwinyi Zanzibar kwa ajili ya ufadhili wa shughuli za wiki ya msaada wa kisheria, na kudhamini mbio za Afrika Mashariki zinazolenga kuzuia vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia pamoja na kuchimba kisima cha maji safi na salama kwa wananchi wa Shehia ya Donge Muwanda.

***Sekta ya Madini***

99. **Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi imeendelea kutumia mfumo wa usimamizi wa Madini ambao unamwezesha mwananchi popote alipo kufanya maombi ya kusafirisha na kuhamisha Maliasili Zisizorejesheka, mfumo huo umeongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wananchi, kupunguza mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali. Aidha, Wizara kupitia Idara ya Nishati na Madini imeendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya matumizi ya mfumo huo pamoja na matumizi bora ya madini ya ujenzi.

100. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na manunuzi ya vifaa vya upimaji na utambuzi wa madini kwa matumizi katika Bandari na Uwanja wa Ndege ili kudhibiti uingizaji na usafirishaji wa madini nchini na kuzuia upotevu wa mapato ya Serikali. Miongoni mwa vifaa hivyo ni; "*Melta Toledo Balance – JET3002G/00, SmartPro Gem-Eye1 Gemstones Tester na XRF Four Element Analysis"*.

101. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na juhudi za kutafuta mbadala wa madini ya ujenzi, ili kupunguza kasi ya uchimbaji wa madini ya ujenzi nchini, katika kufanikisha hilo kwa malengo ya muda mrefu Wizara inaendelea na hatua za manunuzi za kumpata Mshauri elekezi ambaye ataishauri Serikali juu ya matumizi mbadala ya madini ya ujenzi ambayo yataendana na mazingira ya visiwa vyetu na urahisi wa kupatikana.

102. **Mheshimiwa Spika,** aidha, Wizara imefanya utafiti juu ya uingizaji wa madini ya ujenzi kutoka Tanzania bara ambapo taratibu zinaendelea za kuweka utaratibu wa kuingiza madini hayo nchini pamoja na kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya uchimbaji wa madini ya ujenzi, ili kuepuka uchimbaji holela ambao ni hatari kwa mazingira yetu.

103. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imesimamia uhuishaji wa mashamba matano (5) yaliyochimbwa na wananchi. Bumbwini misufini zoni tatu (3) na donge mchangani zoni mbili (2). Aidha, Wizara imeshiriki kikamilifu zoezi la upandaji miti katika eneo la Serikali Donge Muwanda, zoezi ambalo Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania alishiriki.

104. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea na doria na kuzifanyia kazi taarifa zinazotolewa na wananchi juu ya uchimbaji haramu katika maeneo yao pamoja na kuwachukulia hatua wale wote wanaobainika kufanya vitendo hivyo. Aidha, Wizara inaendelea kukiimarisha kikosi cha doria kwa kukiongezea nguvu na kukipatia vifaa vya kisasa, ili kuimarisha ufanisi wa majukumu yao.

105. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ikishirikiana na GST, imekamilisha utafiti wa miamba Unguja na Pemba kwa ajili ya ramani ya kijiolojia. Sampuli 75 zimechukuliwa kwa uchunguzi wa jiokemia kuainisha madini na elementi. Matokeo ya awali yanaonyesha uwepo wa miamba bora ya chokaa kwa viwanda, madini tembo katika fukwe za Unguja na miamba inayoweza kuhifadhi maji, mafuta na gesi. Kuna maeneo hatarishi kama Jambiani, Muyuni na Fumba pamoja na vivutio vya utalii kama Kuza Cave, Kuumbi Cave na Kiwengwa Cave.

106. **Mheshimiwa Spika,** aidha, Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya Aseel Group of Companies walifanya utafiti wa awali wa madini ya metali na mawe ya thamani katika kisiwa cha Unguja. Utafiti huo ulianza tarehe 10 Oktoba, 2023 katika maeneo ambayo yameelezwa na wataalamu wa sayansi na madini kuwa yanaweza kuwa na madini. Baadhi ya maeneo yaligunduliwa kuwa na viashiria vya uwepo wa madini ya dhahabu, fedha na chuma na sampuli zimechukuliwa kwa ajili ya uchunguzi wa maabara. Matokeo ya utafiti yataipa Serikali taarifa muhimu zitakazoiwezesha Serikali kufanya maamuzi sahihi.

107. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi, 2023/2024 Wizara imelipa **TZS. 265,436,471** kwa wananchi ambao vipando vyao vimeathirika kutokana na uchimbaji wa Maliasili zisizorejesheka. Vile vile, Wizara imeendelea kulipa fidia **TZS. 655,380,600** kwa wananchi ambao mashamba yao yalichimbwa mchanga na Serikali.

**Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya (WMNM)**

108. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa chini ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti pamoja na Afisi Kuu - Pemba. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Programu hii iliidhinishiwa kutumia jumla ya **TZS. 2,149,570,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na mishahara. Hadi Machi, 2023/2024 programu hii imetumia **TZS. 1,593,410,380** sawa na asilimia **97** ya makadirio ya **TZS. 1,636,646,625**

kwa ajili ya matumizi mengineyo na Mishahara. Wizara kupitia programu hii imetekeleza kazi zake kama ifuatavyo:-

**a) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti**

**109. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kuhakikisha miongozo ya kusimamia upatikanaji wa huduma endelevu za maji, nishati, na madini inazidi kuimarika. Kwa kushirikiana na Mshauri Elekezi kupitia ufadhili wa UNICEF, Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2004, ili kuwa na Sera ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2024 inayoendana na wakati, kuongeza wigo wa uwekezaji kupitia ushirikishwaji wa Sekta Binafsi pamoja na kuimarika kwa huduma za usafi wa mazingira.

**110. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Programu ya Uimarishaji wa Rasilimali za Ndani na Usimamizi wa Maliasili, inaendelea kuandaa Sera ya Madini ya mwaka 2024 pamoja na Sheria kwa lengo la kuwa na miongozo bora kuhusu uingizaji, usafirishaji, uchimbaji, na uimarishaji wa Sekta ya Madini Zanzibar. Rasimu ya Sera hiyo imeshapitiwa katika Kamati Tendaji ya Wizara na maoni ya wadau yanaendelea kujumuishwa ili kuiboresha kabla ya hatua nyingine.

**111. Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kufanya mapitio ya Sera ya Nishati ya Mwaka 2009 na kuandaa Sera mpya ya Nishati ya Mwaka 2024 itayokidhi mahitaji ya sasa na kwenda sambamba na kasi ya teknolojia ya masuala ya nishati. Kukamilika kwa sera hiyo kutapelekea kuandaliwa kwa Sheria ya Nishati ambayo itasimamia miongozo katika Sekta hiyo. Rasimu ya Sera hiyo imeshakamilika na inatarajiwa kuwasilishwa katika Kikao cha Kamati ya Makatibu Wakuu kwa hatua zaidi.

**112. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kufuatilia utekelezaji wa miradi Unguja na Pemba. Lengo la ziara hizo ni kuongeza kasi ya utekelezaji na kukamilika ndani ya wakati uliopangwa kwa mujibu wa makubaliano. Ziara hizo zimefanyika kwa miradi ya Ahueni ya Uviko – 19 na Mradi wa Exim – India. Aidha, Wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaendelea kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mradi wa ZESTA, ili kuhakikisha unakamilika na kuleta tija kwa taifa. Miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Aidha juhudi zinachukuliwa kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati licha ya changamoto zinazoikabili

ambazo hukwamisha kasi ya utekelezaji. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na kutounganishwa kwa wakati miundombinu ya umeme kwa baadhi ya maeneo ya visima, ucheleweshwaji wa uingiziaji wa vifaa vya ujenzi kutoka India na wananchi kuchelewa kulipwa fidia. Wizara inaendelea kuchukua hatua ikiwa pamoja na kuwataka Wakandarasi na Wasimamizi wa miradi kusimamia ipasavyo na kuhakikisha miradi hiyo inakamilika ndani ya wakati uliopangwa.

113. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha usahihi wa Takwimu zinazozalishwa na kukusanywa kupitia Taasisi na Idara, Wizara kwa kushirikina na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imeandaa nyenzo kwa ajili ya kukusanya Takwimu zinazozalishwa. Kupitia nyenzo hiyo itapelekea kuanzishwa kwa Kitabu cha Muhtasari wa Takwimu *"Statistical Abstract"* ambayo italeta tija katika matumizi ya ukuwaji wa maendeleo ya nchi yetu.

114. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeimarisha ushirikiano kupitia vikao vya sekta (SMZ na SJMT). Hatua hii ni moja ya kutekeleza maagizo ya Viongozi wetu Wakuu wa Nchi juu ya umuhimu wa kuendeleza ushirikiano. Kwa upande wa Sekta ya Maji kikao kilifanyika Zanzibar tarehe 30 Agosti, 2023 hadi 02 Septemba, 2023. Kikao hichi kimewezesha kubadilishana uzoefu na kujifunza masuala yanayohusiana na Sekta ya Maji.

115. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Watendaji kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) inaendelea na matayarisho ya kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Tangi la Maji – Kizimkazi. Kukamilika kwa mradi huu kutarahisisha upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa Kizimkazi. Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na manunuzi kwa ajili ya kuipata kampuni yenye uwezo na sifa za kuanza ujenzi wa mradi huo.

### b) Idara ya Uendeshaji na Utumishi

116. **Mheshimiwa Spika,** Idara inaendelea kuratibu, kusimamia maendeleo ya rasilimali watu pamoja na kutekeleza kazi za kila siku za Ofisi ikiwemo; kuimarisha mazingira ya kazi, kuwapatia wafanyakazi stahiki zao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Miongoni mwa stahiki hizo ni pamoja na; mishahara, likizo, malipo baada ya saa za kazi, kutoa ubani kwa wafiwa, malipo ya kujikimu na malazi na mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

117. **Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha utendaji kazi, Wizara imeratibu na kusimamia vikao mbali mbali ikiwemo; vikao vinne (4) vya Kamati Tendaji, vikao vitatu (3) vya Kamati ya Uongozi, vikao vitatu (3) vya Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu wa Awali na Endelevu, vikao 13 vya Bodi ya Zabuni na kikao kimoja (1) cha wafanyakazi ambacho kilijadili mafanikio, changamoto na maendeleo ya wafanyakazi.

118. **Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kuboresha ufanisi wa kazi, hadi Machi, 2023/2024 imeendelea kufanya manunuzi ya vitendea kazi, kulipia huduma za uendeshaji wa Ofisi pamoja na usimamizi wa matengenezo ya vyombo vya usafiri.

**c) Afisi Kuu Pemba**

119. **Mheshimiwa Spika,** katika kusimamia na kuratibu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa upande wa Pemba, Wizara inaendelea na hatua za kuimarisha Mazingira ya kazi kwa Wafanyakazi, pamoja na kuwapatia stahiki zao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

120. **Mheshimiwa Spika,** Afisi Kuu-Pemba ina jumla ya wafanyakazi 50 (wanaume 29 na wanawake 21). Katika kusimamia na kuratibu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa upande wa Pemba, Afisi Kuu-Pemba inaendelea na hatua za kuimarisha mazingira ya kazi kwa wafanyakazi, pamoja na kuwapatia stahiki zao kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Miongoni mwa stahiki hizo ni mishahara, mafunzo ya muda mrefu na mfupi, likizo, malipo ya kujikimu na malazi na stahiki nyenginezo pamoja na kusimamia shughuli zote za uendeshaji wa Afisi Kuu-Pemba.

121. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi, 2023/2024 wafanyakazi nane (8) walikwenda likizo la kawaida, wafanyakazi wawili (2) wamekwenda likizo la Uzazi na wafanyakazi watano (5) wameenda likizo la dharura. Vile vile, wafanyakazi 18 wamenufaika na Mafunzo ya utumiaji wa mfumo wa Ofisi *"E-office"* na Wafanyakazi 12 wamepatiwa mafunzo ya kuthibitishwa kazini (Induction course). Aidha, Afisi Kuu – Pemba imewafanyia tathmini ya Utendaji kazi Wafanyakazi 20 pamoja na kuwapeleka wafanyakazi watatu (3) mafunzo ya Udhibiti na Utunzaji wa taarifa kutoka kitengo cha Tehama, Masjala na kitengo cha Takwimu.

122. **Mheshimiwa Spika,** Afisi Kuu - Pemba imeendelea kufanya ufuatiliaji wa Miradi ikiwemo Miradi ya Maji inayotekelezwa kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), Miradi ya umeme kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) pamoja na vituo vya mafuta vinavyodhibitiwa na ZURA.

123. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi, 2023/2024 Afisi Kuu Pemba imefanya doria 92 na kukamata makosa yakiwemo; kusafirisha bila ya kibali Maliasili Zisizorejesheka, kukiuka masharti ya leseni na *"attempting excavation"*. Wahusika wa makosa hayo walitozwa faini kulingana na aina ya makosa yao. Aidha, Afisi Kuu Pemba imeratibu usafirishaji wa maliasili zisizorejesheka katika Kware zote zilizopo Pemba ambapo jumla ya tani 58,888 za Mchanga, 13,946 Kifusi, 28,965 Jiwe, 19,618 Kokoto, 7,816 Tofali, 66 Udongo na 2,174 Vumbi zimesafirishwa.

124. **Mheshimiwa Spika,** Afisi Kuu Pemba imefanikiwa kufanya zoezi la upimaji wa magari yanayochukuwa maliasili zisizorejesheka Mkoa wa Kusini na Kaskazini. Vile vile, katika kuhakisha magari yanayosafirisha maliasili hizo hayapati usumbufu na kufanikisha kazi kwa urahisi, Afisi Kuu Pemba imeboresha barabara kwa kuweka kifusi katika maeneo ya Kiungoni, Tumbe Chwaka, Saninga na Uwandani.

125. **Mheshimiwa Spika,** Afisi Kuu Pemba ilifanya kikao na Makarani mapato wa vituo vya usimamizi wa Maliasili zisizorejesheka kwa lengo la kujadili changamoto, fursa, mikakati na namna kitengo kitakavyoimarisha utendaji na kuongeza mapato. Aidha, katika kutatua changamoto za waathirika wa uchimbaji wa Maliasili zisizorejesheka, Wizara imelipa fidia kwa waathirika wa vipando katika shamba la Mchanga la Uondwe. Vile vile, imewajengea uelewa wafanyakazi wa vituo vya kudhibiti Maliasili zisizorejesheka juu ya athari za uhujumu uchumi.

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO CHINI YA (WMNM)

126. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi, 2023/2024 Wizara ya Maji, Nishati na Madini imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo na kupata mafanikio yafuatayo: -

i. **Programu ya Miundombinu ya Maji**

127. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Miundombinu ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ilipangiwa jumla ya **TZS. 10,500,000,000.** Hadi Machi, 2023/2024 jumla ya **TZS. 2,609,201,482** zimepatikana, sawa na asilimia **24.85** ya makadirio. Fedha hizo zilitumika kununua vifaa vya maji, kujenga vibanda vya kuendeshea pampu, kununua mita za maji na kulipa fidia kwa wananchi walioathiriwa na ujenzi wa miundimbinu ya maji katika maeneo ya Upenja, Chaani, Mchangani - shamba, Chumbuni, Makunduchi, Dunga Jumba la Mawe na Bungi.

ii. **Mradi wa Uhuishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar**

128. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu una lengo la kuongeza hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Shehia 36 zilizopo katika Wilaya za Unguja. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mradi ulipangiwa jumla ya **TZS. 29,658,666,000.** Kati ya fedha hizo, **TZS. 11,154,964,000** ni kutoka Serikalini na **TZS. 18,503,702,000** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi Machi 2023/2024, jumla ya **TZS. 21,669,450,854** zimepatikana (**TZS. 20,560,756,804** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na **TZS. 1,108,694,050** kutoka Serikalini) sawa na asilimia **73.06** ya fedha zilizopangwa. Shughuli zilizotekelezwa ni uchimbaji wa visima 64 vyote vikiwa vimekamilika. Ujenzi wa Matangi 15 umefikia asilimia **96** na kazi zilizobaki ni kufunga mfumo wa Tehama *"HMT",* kupeleka miundombinu ya umeme, kuweka taa, kutengeneza njia za ndani na kusawazisha eneo *"leveling"*. Ulazaji wa mabomba kwa kilomita 453.7 umefikia asilimia 97 na kazi iliyobaki ni kumalizia kulaza bomba maeneo ya Mkorogo na Mfenesini. Ujenzi wa Ofisi umekamilika kwa asilimia 100. Aidha, malipo ya fidia yamefanyika kwa wananchi katika maeneo ya Mfenesini, Dole, Kizimbani na Kijichi.

iii. **Mradi wa Uimarishaji wa Usambazaji Maji Zanzibar kupitia fedha za Ahueni ya Uchumi na Ustawi wa Jamii UVIKO - 19 kwa Upande wa ZAWA**

129. **Mheshimiwa Spika,** ili kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama Unguja na Pemba, Serikali ilitenga jumla ya **TZS. 34,200,000,000** kupitia fedha za mkopo nafuu kutekeleza Programu ya Kuhuisha Ustawi wa Uchumi na Kijamii kutokana na Athari za UVIKO-19 kutoka Shirika la

Fedha Duniani (IMF) kwa kazi za uchimbaji wa visima (38), ukarabati wa visima (36), ununuzi na ufungaji wa pampu 51, uboreshaji na ubadilishaji wa mtandao chakavu kwa masafa ya kilomita 319, ujenzi wa Matangi (10), ukarabati wa Matangi (3) na ujenzi wa vibanda 51. Hadi Machi, 2023/2024 kazi zilizofanyika ni uchimbaji wa visima 38 (Unguja visima 11 na Pemba visima 27), ujenzi wa Matangi 10 (Unguja Matangi 5 na Pemba matangi 5), uchimbaji wa misingi na ulazaji bomba na kazi ya ujenzi wa vibanda 51 ambayo imekamilika kwa asilimia 100. Hata hivyo kazi ya ulazaji mabomba ambayo inafanywa na ZAWA inaendelea kwa baadhi ya maeneo.

**iv. Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Usambazaji Maji Zanzibar (JICA)**

130. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu haukutengewa fedha kutoka Serikalini kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Aidha, TZS.9,961,650,000 zilipangwa kutumika kutoka kwa Muhisani ambapo hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **TZS 3,500,000,000** sawa na asilimia **35.13** zimepatikana na kutumika kwa malipo ya Mshauri Elekezi.

**v. Programu ya Utambuzi na Usajili wa visima binafsi**

131. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inatekelezwa kwa pamoja baina ya Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF) kwa gharama za **TZS. 75,000,000**. Programu hii inafanya kazi ya utibabu wa maji kwa kutumia *"chlorine",* Usimamizi na uangalizi wa ubora wa maji pamoja na utambuzi wa visima vya watu binafsi Zanzibar. Hadi Machi, 2023/2024, jumla ya **TZS. 57,030,000** sawa asilimia **76.04** ya makadirio zimepatikana na kutumika kwa kazi hizo.

**vi. Mradi wa Usalama wa Maji Zanzibar (KfW)**

132. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZAWA imeshirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) na kufanikiwa kupata fedha **EURO 660,000** kwa ajili ya kufanya Upembuzi Yakinifu wa kujua hali ya upatikanaji wa maji Unguja na Pemba. Ripoti ya Awali ya Upembuzi Yakinifu imewasilishwa na matumizi ya fedha zote yamefanyika. Hatua iliyopo ni kupatiwa kibali cha kuendelelea na utekelezaji wa Mradi kwa kuanzia na kupata Mshauri Elekezi wa kufanya usanifu wa Mradi hatimaye kupatikana nyaraka za kumpata mkandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi kwa Pemba.

vii. **Mradi wa Uhuishaji na Usambazaji Maji India (India -Exim 35)**

133. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa baina ya SMZ/ZAWA na Benki ya Exim-India kwa gharama za Dola za Kimarekani **35,000,000,000** kwa ajili ya uimarishaji wa huduma za maji endelevu Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Mradi ulipangiwa kutumia jumla ya **TZS 14,235,000,000** kati ya fedha hizo **TZS 2,850,000,000** kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na **TZS 11,385,000,000** kutoka kwa Muhisani. Hadi kufikia Machi 2024 hakuna fedha zilizopatikana.

viii. **Mradi wa Uhuishaji na Usambazaji Maji *(National Energy Center- NEC)***

134. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu tayari unaendelea na utekelezaji kupitia Wakandarasi kutoka Kampuni ya *"NEC"* katika eneo la Kaskazini Unguja na Serikali ipo katika hatua za utafutaji wa mwekezaji kwa upande wa Kusini Unguja na Pemba.

ix. **Mradi wa Usalama wa Maji na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi Mijini- Unguja na Pemba**

135. **Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unafadhiliwa kupitia Shirika la Maendeleo la Ujerumani *"GIZ"* kwa lengo la kusimamia usalama na upatikanaji wa maji nchini kwa kuzingatia maeneo Makuu Matatu; kuisaidia Wizara ya Maji, Nishati na Madini katika usimamizi wa mikakati na miongozo kutokana na mageuzi yaliyopo, kuanzisha mfumo jumuishi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa kimazingira pamoja na kusaidia Mamlaka ya Maji Zanzibar kuweza kujiendesha kibiashara. Hatua iliyofikiwa kwa sasa ni kuajiri washauri elekezi kwa ajili ya utekelezaji.

x. **Mradi wa Mabadiliko ya Sekta ya Nishati na Upatikanaji wa Huduma ya Umeme *Zanzibar (ZESTA)***

136. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa ZESTA unatekelezwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia wa Dola za Kimarekani milioni 142 kupitia WMNM na ZECO. Mradi umeanza mwaka 2021 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2027 ukiwa na lengo la kuimarisha Sekta ya Umeme nchini kwa kukarabati miundombinu, kujenga line kubwa ya usafirishaji umeme (132kV) kutoka Welezo hadi Ubago, Makunduchi hadi Matemwe kwa Unguja pamoja na ujenzi wa vituo viwili vya kupozea umeme katika maeneo ya Makunduchi na Welezo. Vile vile, mradi huu utajenga mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia nishati ya jua kwa

kiwango cha megawati 18 ambapo mtambo huo pia utajumuisha uhifadhi wa umeme huo kwa kiwango cha megawati 40 kwa saa.

137. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 mradi umepangiwa kutumia Jumla ya Dola za Kimarekani 20,841,357.88 kwa upande wa ZECO na Dola za Kimarekani 4,334,059.79 kwa upande wa Wizara. Hadi Machi 2023/2024, mradi kupitia ZECO umetumia jumla ya Dola za Kimarekani 1,554,915.15 sawa na asilimia 7.46 na kupitia Wizarani umetumia Dola za Kimarekani 1,213,471.30 sawa na asilimia 27.99.

138. **Mheshimiwa Spika,** hadi Machi, 2023/2024 shughuli zilizotekelezwa kupitia mradi huu ni zifuatazo: -

**a. Uendelezaji wa uzalishaji umeme kwa kutumia nishati jadidifu ya jua (Solar pv).**

Shughuli hii ni kufanya Upembuzi yakinifu wa kituo cha kufua umeme kwa kutumia nishati ya jua Makunduchi. Kituo kitakuwa na uwezo wa Megawati 18 na kufunga kihifadhio chenye uwezo wa 40MWh katika kituo cha umeme Mtoni. Kihifadhio hiki kitaimarisha upatikanaji wa umeme wakati wa mahitaji makubwa hasa nyakati za jioni ambapo kumekuwa na upungufu wa umeme.

139. **Mheshimiwa Spika,** Mshauri Elekezi, Ms GOPA Intec ya Ujerumani ameingia mkataba na ZECO tarehe 6 Julai 2023 na amekamilisha nyaraka kwa kazi za awali ikiwa pamoja na uwekaji wa uzio eneo la kituo cha kufua umeme wa jua Makunduchi, kufanya usanifu wa eneo na ujenzi wa barabara kwa ajili ya ufikiaji wa eneo la kufua umeme wa jua. Mshauri elekezi anaendelea kukamilisha Upembuzi yakinifu wa solar pv na kihifadhio. Mkataba na kampuni hii ni wa awamu mbili, ya kwanza; ni miezi sita (6) kwa ajili ya kuweka mazingira ya utayari na ya awamu ya pili ni miezi 18 kwa ajili ya ujenzi pamoja na uendeshaji.

**b. Uimarishaji wa njia za kusafirisha na kusambaza umeme katika kisiwa cha Unguja na vituo vya kupozea na kutawanya umeme**

140. **Mheshimiwa Spika,** kazi zilizopangwa ni pamoja na ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 132 yenye urefu wa takribani kilomita 100 kutoka Welezo hadi Ubago na kutoka Ubago kwenda Makunduchi na Ubago hadi Matemwe. Kazi hizi zinajumuisha ujenzi wa kituo kimoja cha kutawanya umeme katika eneo la Welezo na vituo vya kupozea umeme vya misongo

ya kilovoti 132/33 katika maeneo ya Makunduchi na Matemwe. Hatua zilizofikiwa ni kuwa Mshauri Elekezi WAPCOS kutoka India alisaini mkataba wa miezi 36 Mei 5, 2023 ikiwa ni pamoja na kazi ya usimamizi wa ujenzi wa njia ya umeme na vituo vya Welezo, Makunduchi na Matemwe na kazi hiyo itaanza mara tu baada ya hatua za kukamilisha taratibu za manunuzi za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa njia hiyo ya umeme.

c. **Ufungaji kituo cha uendeshaji (Supervision Control and Data Acquisition - SCADA) wa mifumo ya umeme kwa ajili ya misongo ya umeme ya kilovoti 132, 33 na 11**

141. **Mheshimiwa Spika,** shughuli hii itahusisha ujenzi wa jengo la SCADA litajengwa katika kituo cha umeme Mtoni. Mshauri Elekezi, Ms GOPA Intec ya Ujerumani ameingia Mkataba na ZECO kwa ajili ya kazi tarehe 05 Mei 2023. Mkataba huu ni wa miezi 36 ukihusisha na usimamizi wa ujenzi wa kituo cha SCADA.

d. **Uboreshaji wa njia za usambazaji umeme katika Mji Mkongwe, uendelezaji wa njia mpya za misongo ya kilovoti 33 na 11 katika visiwa vya Unguja na Pemba**

142. **Mheshimiwa Spika,** shughuli hii itahusisha kazi ya kuwaunga wateja wapya 70,000 katika visiwa vya Unguja na Pemba chini ya ufadhili wa banki ya Dunia katika mradi wa ZESTA. ZECO tayari imesaini Mkataba na Mshauri elekezi WAPCOS tarehe 15 Novemba 2023 na kampuni inaendelea na kazi ikiwa pamoja na kukamilisha nyaraka za manunuzi ya utekelezaji wa mradi.

e. **Uunganishaji wa mifumo ya utayarishaji wa bili za malipo kwa ZECO**

143. **Mheshimiwa Spika,** hatua za manunuzi kw ajaili ya kuipata kampuni ya kutekeleza kazi hii zinaendelea ambapo mkataba unatarajiwa kusainiwa ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni 2024.

f. **Tathmini ya fidia kwa waathirika wa mradi na kimazingira wa njia ya umeme wa mkondo wa 132 kv**

144. **Mheshimiwa Spika,** ripoti ya fidia kwa waathirika wa Mradi imekamilika na Benki ya Dunia imeridhia malipo ya fidia ya **TZS 19 Bilioni**. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inalipa fidia hizo. Fedha za fidia zimeshapatikana na malipo kwa waathirika yanaendelea kufanyika.

**g. Utafiti wa Popo na Ndege katika njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 132**

145. **Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu wa utunzaji wa mazingira, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Dunia imefanya utafiti wa Popo na Ndege katika njia ya kusafirisha umeme itakayojengwa, ili kupunguza athari za umeme zitakazoweza kuwapata. ripoti ya mwisho ya utafiti huo tayari imeshawasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kuidhinishwa ili kundelea na hatua nyengine za utekelezaji.

**h. Mshauri Elekezi wa masuala ya mazingira, jamii na usalama kazini**

146. **Mheshimiwa Spika,** katika kukidhi matakwa ya Benki ya Dunia ZECO imeingia Mkataba tarehe 5 Mei 2023 na Mshauri Elekezi, *Newtech Group Ltd* kutoka Sudan ambaye anaendelea na kazi kwa ajili ya ushauri wa masuala ya mazingira, jamii na usalama kazini

**i. Utekelezaji wa kipengele cha jinsia**

147. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Mpango Kazi wa Miaka Mitano wa Jinsia, mradi wa ZESTA umetoa ufadhili wa masomo ya muda mrefu kwa ngazi ya shahada ya kwanza na ya pili kwa wafanyakazi wanawake 22 kwa mwaka wa masomo 2023/2024. Wanafunzi hao wanaendelea na muhula wa pili wa masomo. Aidha, mradi unaendelea na utoaji wa mafunzo kazini kwa wanafunzi wanawake na jumla ya wanafunzi 29 wanaendelea na mafunzo hayo katika Taasisi za ZECO, ZURA na Idara ya Nishati.

**j. Kuajiri Mtaalamu wa Kiuchumi wa Udhibiti wa Huduma za Nishati**

148. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia imeingia makubaliano ya mkataba wa ajira wa miaka mitatu kuanzia tarehe 03/07/2023 na Mtaalamu wa Kiuchumi wa udhibiti wa huduma za nishati. Mtaalamu ameshanza utekelezaji wa mpango kazi na kuijengea uwezo Taasisi ya ZURA. Kwa sasa mtaalamu huyo kwa kushirikiana na ZURA anaendelea na kazi ya kupitia na kuandaa gharama ya uendeshaji wa huduma ya umeme ambayo ipo katika hatua ya ukusanyaji wa taarifa.

**k. Kuajiri Mtaalamu wa Kiufundi wa Huduma za Nishati**

149. **Mheshimiwa Spika,** Mradi kupitia Mtaalamu wa kiufundi wa huduma za nishati anaendelea kutekeleza mpango kazi na kuimarisha uwezo wa

Taasisi ya ZURA. Pia, mtaalamu anaendelea kuongoza ZURA katika maandalizi ya msimbo wa gridi (grid code) ambayo ni nyaraka muhimu katika kuinganisha gridi ya Taifa.

**l. Kuandaa nyaraka za kuimarisha sekta ya nishati**

150. **Mheshimiwa Spika,** Mradi umekamilisha taratibu za kusaini mkataba tarehe 28/08/2023 na kampuni ya EXERGIA Energy and Environment kutoka Ugiriki kwa ajili ya kuandaa nyaraka za Mpango Mkuu wa Matumizi sanifu ya Umeme Zanzibar. Kampuni hiyo tayari imekamilisha maandalizi ya Rasimu ya Mpango huo na hatua inayofuata ni kuwasilishwa katika vikao vya uongozi wa Wizara ili kupatiwa maoni.

151. **Mheshimiwa Spika,** Wizara katika kutekeleza majukumu yake imekamilisha taratibu za manunuzi juu ya mradi wa tathmini ya uwezo wa kitaalam katika sekta ya nishati. Wizara tayari imesaini mkataba na kampuni ya CRIS Limited kutoka India kwa ajili ya kufanya tathmini ya mahitaji ya kitaalamu (Capacity need assessment) katika sekta ya nishati. Mkataba huo umesainiwa tarehe 17/08/2023. Kampuni hiyo tayari imeshandaa rasimu ya ripoti baada ya ukusanyaji wa taarifa za mahitaji katika taasisi za Nishati. Rasimu hiyo imewasilishwa kwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kutolewa maoni.

**m. Mpango wa Umeme Zanzibar *(Integrated Resource Plan)***

152. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia imekamilisha taratibu za kusaini mkataba tarehe 8/09/2023 na kampuni ya *Economic Consulting Associates* kutoka Uingereza kwa ajili ya kuandaa Mpango Mkuu wa Mahitaji ya Umeme wa miaka ishirini. Kampuni hiyo imekamilisha zoezi la ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya kufanya makadirio ya mahitaji na matumizi ya umeme. Aidha, kampuni hiyo inaendelea na zoezi la kufanya makadirio na rasimu imeshawasilishwa kwa lengo la kupata maoni.

**xi. Mradi wa Usambazaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Umeme Zanzibar kupitia fedha za Ahueni ya Uchumi na Ustawi wa Jamii UVIKO-19 kwa Upande wa ZECO**

153. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia ZECO imepatiwa jumla ya **TZS. 11.469 bilioni** za ununuzi wa vifaa vya umeme kwa lengo la kuwafikishia huduma ya umeme wananchi wa Unguja na Pemba. Vifaa hivyo ni; nguzo,

mita "wall clamps, Galvanized Pipe 2m (Roof Pole), Suspension Clamp 4x50mm2, Tee-Off (Connector) na (Pc Clamp) 25-95mm2." Fedha za mradi huu zimetuika na kazi imekamilika.

## 5.0 MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

154. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imejipangia kutekeleza bajeti yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kuimarisha miundombinu ya usambazaji wa huduma ya umeme na maji;

ii. Kudhibiti wizi wa umeme, miundombinu ya maji pamoja na uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji;

iii. Kuimarisha nyenzo za udhibiti wa huduma za maji na nishati;

iv. Kufanya tafiti kwa lengo la kuimarisha huduma za sekta zinasimamiwa na Wizara;

v. Kuwatambua, kuwasajili na kuwafungia mita wateja wapya na wazamani wanaoopata huduma ya maji; na

vi. Kuimarisha upatikanaji wa huduma ya Maji, huduma ya Nishati na huduma ya Madini kwa kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati.

155. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Maji, Nishati na Madini itatekeleza vipaumbele hivyo kupitia Programu Kuu tatu (3) na Programu Ndogo sita (6) zifuatazo: -

### A. Programu Kuu PN0301: Usimamizi wa Huduma za Maji

Programu hii itatekelezwa kupitia Programu Ndogo moja (1) ambayo ni:-

i. Usimamizi na Uratibu wa Huduma za Maji, na

156. **Mheshimiwa Spika,** katika kufikia malengo ya Programu hii, Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Maji imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuibua na kusimamia utekelezaji wa shughuli/miradi katika sekta ya maji kitaifa;

ii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Uwekezaji wa Sekta ya Maji Zanzibar (Zan-WIP 2022 – 2027);

iii. Kuhifadhi, kusimamia na kuendeleza rasilimali maji kwa Unguja na Pemba; na

iv. Kusimamia upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama na usafi wa mazingira Unguja na Pemba.

157. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii pia itatekelezwa kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ambayo inajukumu la kusimamia masuala ya maji hapa Zanzibar. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, ZAWA kupitia programu hii imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kutoa elimu kwa wananchi Unguja na Pemba juu ya umuhimu wa kutunza miundombinu ya maji, vyanzo vya maji pamoja na kulipia ada za matumizi ya maji;

ii. Kuendelea kuchimba visima katika maeneo yenye uhitaji;

iii. Kuwatambua, kuwasajili na kuwafungia mita wateja wapya kwa Unguja na Pemba;

iv. Kuendelea kuziba mivujo kwa maeneo yenye uhitaji;

v. Kuendelea kusafisha visima katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba;

vi. Kuwajengea uwezo wafanyakazi 36 wa Mamlaka kwa kuwapatia mafunzo ya Muda mrefu; na

vii. Kukusanya mapato yanahusiana na matumizi ya Maji, Miundombinu pamoja na ada za wanafunzi wa Chuo cha Maji.

158. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) imejipangia kukusanya jumla ya **TZS. 10,870,491,200** kutoka vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni mauzo ya maji na mapato mengineyo. Aidha, Mamlaka imekadiria kutumia jumla ya **TZS. 7,120,491,200** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na **TZS 3,750,000,000** ni mchango wa ZAWA kwa Serikali.

159. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Maji iweze kutekelezwa, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 164,486,943,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara, ruzuku ya mishahara na kazi za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **TZS. 430,720,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, **TZS. 294,214,000** kwa ajili ya mishahara, **TZS. 9,134,300,000** kwa ajili ya ruzuku ya mishahara, na **TZS. 154,627,709,000** kwa ajili ya kazi za miradi ya maendeleo.

**B. Programu Kuu PN0302: Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini.**

Programu hii itakuwa na Programu Ndogo mbili ambazo ni:-

i. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati; na

ii. Programu Ndogo ya Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Madini.

160. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii, imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kutoa elimu ya matumizi ya Nishati Sanifu na Nishati za Kisasa;

ii. Kuandaa na kushiriki mikutano na makongamano ya Kikanda na Kimataifa katika masuala ya nishati;

iii. Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Nishati ya Mwaka 2009 na kuendeleza juhudi za upatikanaji wa Umeme na Nishati mbadala;

iv. Kusimamia utafutaji wa vyanzo mbadala vya nishati pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa nishati hizo;

v. Kusimamia utekelezaji wa miradi ya nishati;

vi. Kuandaa na kushiriki mikutano na makongamano ya Kikanda na Kimataifa katika masuala ya madini; na

vii. Utoaji wa Elimu kwa wananchi juu ya upatikanaji wa maliasili zisizorejesheka.

161. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii pia itatekelezwa kupitia Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA).

**a) Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO)**

162. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kupitia programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa mapato;

ii. Kuongeza ubora wa huduma kwa wateja;

iii. Kuwaunganishia wateja wapya wa umeme wapatao 38,400

iv. Kudhibiti wizi wa umeme;

v. Kuimarisha miundombinu ya usambazaji wa umeme;

vi. Kuandaa mpango wa mafunzo, miongozo ya kazi na ushirikishwaji wa wafanyakazi katika kutoa maamuzi;

vii. Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi;

viii. Kusimamia utendaji kazi wa Shirika;

ix. Kusimamia Matengenezo ya kawaida ya miundombinu ya usafirishaji na usambazaji wa umeme; na

x. Uendelezaji wa upatikanaji wa huduma ya umeme wa uhakika.

163. **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) linatarajia kukusanya jumla ya **TZS. 215,981,245,477** kupitia vyanzo vyake vya mapato ambavyo ni mauzo ya umeme, mapato ya huduma nyenginezo, mchango wa Serikali na makusanyo ya madeni ya nyuma ya wateja. Shirika limekadiria kutumia jumla ya **TZS. 215,895,971,479** kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida na kazi za maendeleo. Aidha, ifikapo tarehe 30 Juni, 2025 Shirika linatarajia kupata bakaa ya jumla ya **TZS. 85,273,999.**

b) **Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA)**

**164. Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, ZURA kupitia programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuimarisha nyenzo za udhibiti wa huduma za maji na nishati;

ii. Kuimarisha upatikanaji bora, endelevu na salama wa huduma za maji na nishati;

iii. Kufanya tafiti kwa lengo la kuimarisha huduma za sekta zinazosimamiwa na Wizara;

iv. Kuimarisha mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi;

v. Kuboresha uwezo wa taasisi wa kudhibiti huduma za maji na nishati; na

vi. Kutoa elimu pamoja na kuongeza uelewa kwa umma kuhusu amMlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati.

**165. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, ZURA imejipangia kukusanya jumla ya **TZS. 26,448,099,500** kutokana na tozo la Mamlaka "Regulatory Levy" inayotokana na mafuta, mapato ya leseni na mapato mengineyo. Aidha, imekadiria kutumia jumla ya **TZS. 26,448,099,500** kwa ajili ya kazi za kawaida, Maendeleo na Mchango wa Mfuko Mkuu wa Serikali. Kati ya fedha hizo, **TZS. 8,242,842,097** kwa ajili ya kazi za kawaida, **TZS. 3,205,257,403** kwa ajili ya mishahara, **TZS. 5,000,000,000** kwa ajili ya kazi za Maendeleo na **TZS. 10,000,000,000** kwa ajili ya Mchango wa Serikali.

c) **Idara ya Nishati na Madini**

**166. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara kutokana rasilimali zisizorejesheka, imepangiwa kukusanya jumla ya TZS. 15.622 Bilioni. Makusanyo hayo yanatokana na maombi ya vibali, ada, leseni na faini zitokanazo na malipo ya rasilimali hizo.

**167. Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Usimamizi wa Huduma za Nishati na Madini iweze kutekelezeka, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025,

naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 212,358,150,000** kwa matumizi mengineyo, mishahara na kazi za maendeleo. Kati ya fedha hizo, **TZS. 251,400,800** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **TZS. 850,880,000** kwa ajili ya mishahara na **TZS. 211,255,869,000** kwa ajili ya kazi za Maendeleo.

**C. Programu Kuu PN0303: Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM.**

Program hii itakuwa na Programu ndogo tatu ambazo ni: -

i. Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa WMNM;

ii. Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti wa WMNM; na

iii. Programu Ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za WMNM -Afisi Kuu Pemba.

**168. Mheshimiwa Spika,** Programu hii imejipangia kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuandaa vikao vya Kamati ya Uongozi, Kamati Tendaji, vikao vya Bodi ya Zabuni na vikao vya Wafanyakazi;

ii. Kutoa huduma za uendeshaji wa Ofisi katika Wizara ya Maji Nishati na Madini;

iii. Kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu, muda mfupi na ya ndani ikiwa pamoja na uelewa wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma pamoja na maadili ya kazi;

iv. Kufanya ukaguzi wa hesabu za awali na endelevu katika ofisi na vikao vya Kamati ya ukaguzi;

v. Kuandaa na kuratibu Mipango na Mikakati ya WMNM ikiwa pamoja na miradi ya maendeleo na kusimamia Utekelezaji wake;

vi. Kufanya ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za WMNM;

vii. Kufanya utafiti juu ya kutathimni athari zitokanazo na uchimbaji wa Maliasili zisizorejesheka Unguja na Pemba;

viii. Kuandaa na kuratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya WMNM;

ix. Kukusanya na kuchambua takwimu za utekelezaji wa shughuli za WMNM;

x. Kuratibu na kukuza mashirikiano ya Kisekta na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za Wizara; na

xi. Kuandaa MTEF/PBB, Mpangokazi, Mpango wa manunuzi, Nominal roll na Hotuba ya Bajeti ya WMNM.

169. **Mheshimiwa Spika,** ili Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya Wizara iweze kutekelezeka, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya **TZS. 2,742,985,000** kwa matumizi ya kazi za kawaida na mishahara. Kati ya fedha hizo, **TZS.1,093,079,000** kwa ajili ya matumizi kawaida na **TZS. 1,649,906,000** kwa ajili ya mishahara.

## 6.0 MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

170. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Wizara ya Maji, Nishati na Madini kutekeleza Programu zake na kazi zilizopangwa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Programu za Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa Fungu N03 lenye jumla ya **TZS.379,588,078,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo, mishahara, ruzuku ya mishahara na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **TZS. 1,775,200,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **TZS. 2,795,000,000** kwa ajili ya Mishahara, **TZS. 9,134,300,000** kwa ajili ya Ruzuku ya mishahara na **TZS. 365,883,578,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wa fedha zitakazotumika kwa utekelezaji wa kila Programu umeainishwa katika **Kiambatisho Namba.7.**

Vile vile, naomba idhini ya kukusanya **TZS. 15,622,666,000** kutoka katika vyanzo mbali mbali vya mapato yatokanayo na maliasili zisizorejesheka.

## 7.0 HITIMISHO

171. **Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyengine naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa namna anavyotekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025 kwa vitendo. Sote ni mashahidi kuwa mambo mengi aliyoahidi kuyatekeleza katika kipindi hiki tayari ameshayatekeleza. Ameidhihirishia Dunia kwamba *"Muungwana ni vitendo"*. Natoa wito kwetu sisi Wawakilishi wa wananchi tutekeleze ahadi tulizoahidi katika Majimbo yetu, ili tuungane na Mheshimiwa Rais wetu mpendwa katika kuwatumikia wananchi waliotuchagua na kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 - 2025.

172. **Mheshimiwa Spika,** mimi binafsi namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana hii. Naahidi kuwa muaminifu na mtiifu kwake na kuendelea kufanya kazi kwa ufanisi, uadilifu na uaminifu, ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

173. **Mheshimiwa Spika,** aidha, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Zawadi Amour Nassor Naibu Waziri, Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa muda mfupi tangu ateuliwe kushika nyadhifa hii, kwa namna anavyochapa kazi kizalendo zaidi na kunisaidia katika kutekeleza majukumu ya kuiongoza Wizara hii inayogusa maisha ya kila mwananchi wa Zanzibar.

174. **Mheshimiwa Spika,** katika kuandaa Hotuba hii naomba kumpongeza kwa dhati kabisa Katibu Mkuu Ndugu Joseph John Kilangi kwa jinsi anavyonipa ushirikiano katika kutekelezaji majukumu yangu ya kusimamia Wizara ya Maji, Nishati na Madini hadi kuwasilisha Hotuba hii mbele ya Baraza lako Tukufu. Pia, kiupekee napenda kuwapongeza watendaji wengine wote wa Wizara hii kwa ushirikiano wao, akiwemo Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mwanajuma Majid Abdullah, Wakurugenzi Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi wa Idara za Wizara pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara kwa ujumla.

175. **Mheshimiwa Spika,** kwa hakika ushirikiano wao mzuri na uchapaji kazi mkubwa umesaidia kuweza kuiongoza Wizara hii na kutekeleza majukumu yangu kwa uweledi katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Zanzibar

wanafaidika na huduma za maji safi na salama, Nishati nafuu na ya uhakika pamoja na upatikanaji wa maliasili zisizorejesheka kwa shughuli mbali mbali za kijamii na kiuchumi.

176. **Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue nafasi hii kushukuru na kuthamini michango na ushirikiano kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ndani na nje ya nchi wakiwemo Taasisi ya Ufuatiliaji wa Utendaji Serikalini (PDB), Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), CRDB Benki, Benki ya Exim ya INDIA, Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW), Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa (WB na IMF), Umoja wa Ulaya (EU) pamoja na Taasisi na Mashirika mengine ya Kimataifa ya maendeleo yakiwemo JICA (Japan), GWPSA, GWPTZ, GiZ (Ujerumani), NEC, NORAD (Norway), UNICEF, SIDA (Sweden), UNDP na Wadau wengine wote wa maendeleo.

177. **Mheshimiwa Spika,** shukrani zangu za dhati nazitoa tena kwa wananchi wangu wa Jimbo la Chake Chake ambao kwa muda wote wameendelea kuniamini na kuniunga mkono katika kuimarisha maendeleo ya Jimbo na Taifa kwa ujumla. Pia, nawashukuru kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya Jimbo na Kitaifa na wakati mwingine kunivumilia kwa kukosa huduma yangu ninapokuwa nikitekeleza majukumu ya kitaifa. Niendelee kuwaahidi na kuwahakikishia kuwa nitazidi kuwatumikia kwa kasi zaidi kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia katika kuleta maendeleo ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

178. **Mheshimiwa Spika,** mwisho naomba sasa nichukue fursa hii adhimu kuishukuru kwa dhati familia yangu pamoja na watoto wangu kwa kunivumilia, kuniunga mkono na kuniombea kwa Mwenyezi Mungu, ili niweze kutekeleza majukumu yangu.

179. **Mheshimiwa Spika,** nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waipokee, waijadili, kutushauri na hatimae waipitishe Bajeti hii.

180. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**(Mheshimiwa Shaib Hassan Kaduara)**
**Waziri wa Maji, Nishati na Madini Zanzibar**

## Kiambatisho Namba 1: Mapitio ya Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

| PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO | TAASISI | MATUMIZI | BAJETI ILIYOPANGWA HADI MACHI, 2024 "000" | | | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI, 2024 "000" | | | % YA FEDHA ZILIZOPATIKANAKWA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | SMZ | WAHISANI | JUMLA | SMZ | WAHISANI | JUMLA | |
| Usimamizi wa huduma za Maji | Kusimamia Huduma na Upatikanaji wa Maji Safi na Salama | Idara ya Maendeleo ya Maji | Fedha za Matumizi Mengineyo | 113,255,000 | | 113,255,000 | 65,800,156 | | 65,800,156 | 58 |
| | | | Fedha za Mishahara | 187,516,500 | | 187,516,500 | 137,191,290 | | 137,191,290 | 73 |
| | | | Ruzuku ya Mshahara | 4,397,625,000 | | 4,397,625,000 | 6,417,357,108 | | 6,417,357,108 | 146 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **4,698,396,500** | **-** | **4,698,396,500** | **6,620,348,554** | **-** | **6,620,348,554** | **141** |
| | Kuimarisha huduma za Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) | Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) | Fedha za Miradi ya Maendeleo | 19,091,223,000 | 42,916,521,500 | 62,007,744,500 | 9,010,660,394 | 41,712,720,286 | 50,723,380,680 | 82 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **19,091,223,000** | **42,916,521,500** | **62,007,744,500** | **9,010,660,394** | **41,712,720,286** | **50,723,380,680** | **82** |
| | **Jumla ya Programu Kuu 1** | | | **23,789,619,500** | **42,916,521,500** | **66,706,141,000** | **15,631,008,948** | **41,712,720,286** | **57,343,729,234** | **86** |
| Usimamizi wa huduma za Nishati na Madini | Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati | Idara ya Nishati na Madini | Fedha za Matumizi Mengineyo | 139,170,000 | | 139,170,000 | 37,177,000 | | 37,177,000 | 27 |
| | | | Fedha za Mishahara | 541,722,750 | | 541,722,750 | 585,319,843 | | 585,319,843 | 108 |
| | | Shirika | Fedha za | 18,150,000,000 | 6,726,386,750 | 24,876,386,750 | 13,265,605,370 | 2,768,386 | 13,268,373,756 | 53 |

| PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO | TAASISI | MATUMIZI | BAJETI ILIYOPANGWA HADI MACHI, 2024 "000" | | | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI, 2024 "000" | | | % YA FEDHA ZILIZOPATIKANAKWA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | SMZ | WAHISANI | JUMLA | SMZ | WAHISANI | JUMLA | |
| | | la Umeme Zanzibar (ZECO) | Miradi ya Maendeleo | | | | | | | |
| | | | **Jumla Ndogo** | **18,830,892,750** | **6,726,386,750** | **25,557,279,500** | **13,888,102,213** | **2,768,386** | **13,890,870,599** | **54** |
| | Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Madini | Idara ya Nishati na Madini | Matumizi ya "retention" | 5,250,000,000 | | 5,250,000,000 | 3,679,447,206 | | 3,679,447,206 | 70 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **5,250,000,000** | **-** | **5,250,000,000** | **3,679,447,206** | **-** | **3,679,447,206** | **70** |
| | **Jumla ya Programu Kuu 2** | | | **24,080,892,750** | **6,726,386,750** | **30,807,279,500** | **17,567,549,419** | **2,768,386** | **17,570,317,805** | **57** |
| Uendeshaji na Uratibu wa Mipango ya WMNM | Utawala na Uendeshaji wa WMNM | Utumishi na Uendeshaji | Fedha za Matumizi Mengineyo | 272,908,125 | | 272,908,125 | 118,166,377 | | 118,166,377 | 43 |
| | | | Fedha za Mishahara | 491,859,000 | | 491,859,000 | 691,464,105 | | 691,464,105 | 141 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **764,767,125** | **-** | **764,767,125** | **809,630,482** | **-** | **809,630,482** | **106** |
| | Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti | Idara ya Mipango, Sera na Utafiti | Fedha za Matumizi Mengineyo | 136,977,750 | | 136,977,750 | 178,213,467 | | 178,213,467 | 130 |
| | | | Fedha za Mishahara | 109,580,250 | | 109,580,250 | 161,436,055 | | 161,436,055 | 147 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **246,558,000** | **-** | **246,558,000** | **339,649,522** | **-** | **339,649,522** | **138** |
| | Uratbu wa Utekelezaji wa Shughuli za | Afisi Kuu - Pemba | Fedha za Matumizi Mengineyo | 150,300,000 | | 150,300,000 | 61,000,000 | | 61,000,000 | 41 |
| | | | Fedha za Mishahara | 475,021,500 | | 475,021,500 | 383,130,376 | | 383,130,376 | 81 |
| | | | **Jumla Ndogo** | **625,321,500** | **-** | **625,321,500** | **444,130,376** | **-** | **444,130,376** | **61** |

| PROGRAMU KUU | PROGRAMU NDOGO | TAASISI | MATUMIZI | BAJETI ILIYOPANGWA HADI MACHI, 2024 "000" | | | FEDHA ZILIZOPATIKANA HADI MACHI, 2024 "000" | | | % YA FEDHA ZILIZOPATIKANAKWA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | SMZ | WAHISANI | JUMLA | SMZ | WAHISANI | JUMLA | |
| | WMNM – Pemba | | | | | | | | | |
| | **Jumla ya Programu Kuu 3** | | | **1,636,646,625** | **-** | **1,636,646,625** | **1,593,410,380** | **-** | **1,593,410,380** | **97** |
| | **JUMLA YA FUNGU NO3** | | | **49,507,158,875** | **49,642,908,250** | **99,150,067,125** | **34,791,968,747** | **41,715,488,672** | **76,507,457,419** | **77** |

**Kiambatisho Namba 2: Maeneo yaliyoimarishwa huduma ya umeme kwa kipindi cha Julai 2923 hadi Machi 2024**

| Nam. | Unguja | Nam. | Pemba |
|---|---|---|---|
| 1 | Kiwengwa Mafarasi | 1 | Markaz Magome |
| 2 | Nungwi Saba saba | 2 | Ole Makumbi |
| 3 | Upenja Uwandani | 3 | Mchnga Mrima |
| 4 | Bwejuu kwa Lila | 4 | Markaz Magome |
| 5 | Nungwi Sabasaba | | |
| 6 | Upenja Uwandani | | |
| 7 | Kidoti Ijitimai | | |
| 8 | Kendwa | | |
| 9 | Kijichi Brilliant | | |
| 10 | Bwejuu kwa Lila | | |
| 11 | Makunduchi Kigaeni | | |
| 12 | Kiwengwa Kumba Urembo | | |
| 13 | Kizimkazi Mkunguni | | |
| 14 | Jambiani Hakuna Majiwe | | |
| 15 | Maungani Vijijini | | |
| 16 | Dole Angola | | |
| 17 | Mtoni Matopeni | | |
| 18 | Kiboje | | |
| 19 | Jambiani Kibigija. | | |
| 20 | Tazari. | | |
| 21 | Jozani. | | |
| 22 | Chukwani Sumait. | | |
| 23 | Kwarara | | |
| 24 | Kiembesamaki Garden. | | |
| 25 | Bwejuu | | |
| 26 | Fuoni kwa Chimbeni. | | |
| 27 | Chukwani | | |
| 28 | Kiembesamaki vijijini. | | |
| 29 | Kiembesamaki milimani | | |
| 30 | Nungwi sabasaba | | |
| 31 | Maungani kwa Mazrui | | |
| 32 | Mpendae | | |

## Kiambatisho Namba 3: Hali ya Uingizaji na Matumizi ya Mafuta kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024

| MWEZI | YALIYOINGIZWA/MATUMIZI | PETROLI | DIZELI | MAFUTA YA TAA | BUNKER | JET A-1 | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| JULAI | Yaliyoingizwa | 7,563,159 | 4,161,323 | 125,714 | | 5,708,271 | 17,558,467 |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,378,780 | 5,611,590 | 196,117 | | 4,400,000 | 19,586,487 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 312,626 | 187,053 | 6,537 | | 146,667 | 652,883 |
| AGOSTI | Yaliyoingizwa | 11,240,101 | 6,503,146 | 152,413 | | 3,806,855 | 21,702,515 |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,485,375 | 5,989,025 | 270,301 | | 5,368,000 | 21,112,701 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 305,980 | 193,194 | 8,719 | | 173,161 | 681,055 |
| SEPTEMBA | Yaliyoingizwa | 8,061,011 | 5,455,109 | 0 | | 3,794,262 | 17,310,382 |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,335,322 | 6,014,030 | 162,800 | | 4,004,000 | 19,516,152 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 311,177 | 200,468 | 5,427 | | 133,467 | 650,538 |
| OKTOBA 2023 | Yaliyoingizwa | 10,587,361 | 7,236,221 | 475,149 | | 5,718,965 | 24,017,696 |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,475,528 | 5,209,992 | 192,300 | | 4,092,000 | 18,969,820 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 315,851 | 173,666 | 6,410 | | 136,400 | 632,327 |
| NOVEMBA 2023 | Yaliyoingizwa | 12,407,016 | 8,268,271 | 0 | | 3,862,083 | 24,537,370 |
| | Matumizi kwa mwezi | 8,534,100 | 4,889,759 | 224,400 | | 4,796,000 | 18,444,259 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 275,294 | 157,734 | 7,239 | | 154,710 | 594,976 |
| DISEMBA 2023 | Yaliyoingizwa | 9,717,138 | 7,470,666 | 0 | | 5,713,663 | 22,901,467 |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,880,208 | 5,585,949 | 183,256 | | 5,192,000 | 20,841,413 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 329,340 | 186,198 | 6,109 | | 173,067 | 694,714 |
| JANUARI | Yaliyoingizwa | 9,730,520 | 6,116,490 | 379,311 | | 5,734,524 | 21,960,845 |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,576,314 | 5,968,146 | 212,847 | 1,476,714 | 6,292,000 | 23,526,021 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 319,210 | 198,938 | 7,095 | | 209,733 | 734,977 |
| FEBUARI | Yaliyoingizwa | 8,109,147 | 6,631,645 | 0 | | 4,619,774 | 19,360,566 |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,593,443 | 6,502,359 | 375,976 | 1,186,100 | 4,438,000 | 22,095,878 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 309,466 | 209,754 | 12,128 | | 143,161 | 674,509 |
| MACHI | Yaliyoingizwa | 5,432,081 | 4,976,838 | 89,869 | | 5,676,970 | 16,175,758 |
| | Matumizi kwa mwezi | 9,335,092 | 5,638,418 | 145,824 | 985,350 | 4,092,000 | 20,196,684 |
| | Wastani wa Matumizi kwa Siku | 311,170 | 187,947 | 4,861 | | 136,400 | 640,378 |
| JUMLA YA MAFUTA YALIOINGIZWA KWA | | 82,847,534 | 56,819,709 | 1,222,456 | | 44,635,367 | 185,525,066 |
| JUMLA YA MAFUTA YALIOUZWA KWA | | 84,594,162 | 51,409,268 | 1,963,821 | | 42,674,000 | 184,289,415 |

### Kiambatisho Namba. 4: Bei za mafuta

| BEI ZILIZOTANGAZWA KWA ROBO YA TATU KUANZIA (JANUARI HADI MACHI) 2023/2024 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| MWEZI | TAREHE YAKUTANGAZWA | BEI ILIYOTANGAZWA | | | |
| | | PETROLI | DIZELI | MAFUTA YA NDEGE | MAFUTA YA TAA |
| JANUARI 2024 | 08.01.2024 | 2,893 | 3,101 | 2,825 | 3,200 |
| FEBRUARI 2024 | 08.02.2024 | 2,933 | 3,102 | 2,636 | 3,200 |
| MACHI 2024 | 08.03.2024 | 3,118 | 3,114 | 2,764 | 3,200 |

*Chanzo: ZURA 2024*

### Kiambatisho Namba. 5: Hali ya Uingizwaji na Matumiz ya Gesi kwa Kila Kampuni

| HALI YA UINGIZWAJI NA MATUMIZI YA GESI KWA KILA KAMPUNI | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MWEZI/KAMPUNI | ORXY GAS TANZANIA LIMITED | | LAKE GAS TANZANIA LIMITED | | TAIFA GAS TANZANIA LIMITED | | TP COMPANY LIMITED - V- GAS | | ALNABAHAN GAS SUPPLY -O-GAS | |
| 2023/2024 | UINGIZAJI | MATUMIZI | UINGIZAJI | MATUMIZI | UINGIZAJI | MATUMIZI | UINGIZAJI | MATUMIZI | UINGIZAJI | MATUMIZI |
| JULAI-SEPTEMBA 2023 | 2,073,223 | 2,074,774 | 215,220 | 168,188 | 291,224 | 270,617 | 82,460 | 85,200 | 12,500 | 107,500 |
| OKTOBA-DISEMBA 2023 | 2,182,274 | 2,257,427 | 235,760 | 187,217 | 237,095 | 264,282 | 82,460 | 85,200 | 12,500 | 107,500 |
| JANUARI-MACHI 2024 | 2,381,800 | 2,341,084 | 210,160 | 211,151 | 331,456 | 311,159 | 0 | 0 | 17,500 | 17,500 |
| **JUMLA NDOGO** | **6,637,297** | **6,673,285** | **661,140** | **566,556** | **859,775** | **846,058** | **164,920** | **170,400** | **42,500** | **232,500** |
| | **UINGIZWAJI** | **8,365,632** | | | | | | | | |
| | **MATUMIZI** | **8,488,799** | | | | | | | | |

**Kiambatisho Namba. 6: Idadi na aina ya malalamiko yaliyopokelewa na kutatuliwa**

| AINA | MAELEZO | HATUA ILIYOFIKIWA |
|---|---|---|
| UMEME | Kukosekana kwa Umeme | Lipo katika hatua za kusubiri majibu kutoka ZECO. |
| | Madai ya Fidia kutokanana na Kuunguliwa kwa nyumba na vifaa kwa Mwananchi- Mtambile Pemba | Lipo katika hatua za kusubiri majibu kutoka ZECO. |
| | Madai ya fidia kwa Watoto waliopata ajali ya moto iliyotokana na shoti ya umeme iliyotokea Fumba | Lipo katika hatua za kusubiri majibu kutoka ZECO. |
| **AINA** | **MAELEZO** | **HATUA ILIYOFIKIWA** |
| | Madai ya fidia yaliyotokana na kupita kwa Miundombinu ya Umeme katika Nyumba iliyopo Karakana | Lipo katika hatua za kusubiri majibu kutoka ZECO. |
| GESI | Madai ya fidia yaliyotokana na kuunguliwa kwa Nyumba iliyotokea Jangombe | Lipo katika hatua za kusubiri majibu kutoka M-GAS. |

***Chanzo: ZURA 2024***

**Kiambatisho Namba. 7: Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

| MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA | | | | MATUMIZI YA KAZI ZA MAENDELEO | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO** | **MSHAHARA** | **RUZUKU YA MISHAHARA** | **UENDESHAJI WA OFISI (OC)** | **MAKISIO YA SMZ** | **WAHISANI** | **RUZUKU** | **MAPENDEKEZO 2024/2025** |
| **USIMAMIZI WA HUDUMA ZA MAJI** | **294,214,000** | **9,134,300,000** | **430,720,000** | **43,504,964,000** | **111,122,745,000** | **-** | **164,486,943,000** |
| Usimamizi na uratibu wa Huduma za Maji | 294,214,000 | 9,134,300,000 | 430,720,000 | 43,504,964,000 | 111,122,745,000 | - | 164,486,943,000 |
| **USIMAMIZI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MADINI** | **850,880,000** | **-** | **251,400,800** | **37,000,000,000** | **174,255,869,000** | **-** | **212,358,150,000** |
| Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Nishati | 826,160,000 | | 209,360,000 | 37,000,000,000 | 174,255,869,000 | - | 212,291,389,000 |
| Usimamizi na Uimarishaji wa Huduma za Madini | 24,720,000 | - | 42,040,800 | - | - | - | 66,761,000 |
| **UENDESHAJI NA URATIBU WA MIPANGO YA WMNM** | **1,649,906,000** | **-** | **1,093,079,000** | **-** | **-** | **-** | **2,742,985,000** |
| Utawala na Uendeshaji wa WMNM | 758,354,000 | - | 451,518,000 | - | - | - | **1,209,872,000** |
| Uratibu wa Mioango, sera na Tafiti za WMNM | 149,490,000 | - | 320,183,000 | - | - | - | **469,673,000** |

| MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA | | | | MATUMIZI YA KAZI ZA MAENDELEO | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **PROGRAMU KUU/PROGRAMU NDOGO** | **MSHAHARA** | **RUZUKU YA MISHAHARA** | **UENDESHAJI WA OFISI (OC)** | **MAKISIO YA SMZ** | **WAHISANI** | **RUZUKU** | **MAPENDEKEZO 2024/2025** |
| Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za WMNM - Pemba | 742,062,000 | - | 321,378,000 | - | - | - | **1,063,440,000** |
| **JUMLA KUBWA** | **2,795,000,000** | **9,134,300,000** | **1,775,200,000** | **80,504,964,000** | **285,378,614,000** | **-** | **379,588,078,000** |